# Nipashe

Ijumaa Machi 5, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580510

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


**Waya** ulivyokatisha maisha ya dereva bodaboda kikatili

UKURASA 3



**Operesheni** kunasa wamiliki hewa wa ardhi yatangazwa

UKURASA 3




**Neymar anakaribia kurudi – Pochettino**

UKURASA 20



# Kupiga nyungu rasmi Muhimbili

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**PM ARIDHISHWA KASI KUPAMBANA NA NZIGE**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema ameridhishwa na kazi...

UKURASA WA 5

**MAWAZIRI WAPYA Z'BAR WAAHIDI MAKUBWA**

MAWAZIRI watatu walioteuliwa, jana waliapishwa na Rais wa...

UKURASA WA 7

**SAMIA ATAKA MTOTO WA KIKE AWE KIONGOZI**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amesema serikali...

## Adaiwa kujinyonga kisa ugumu wa maisha

UKURASA 2



Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Lawrance Museru, akitoka kupiga 'nyungu', baada ya kuzindua kibanda maalum cha kujifukiza kwa ajili ya kujikinga na Covid-19, hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store





# Mbinu kubaini 'sanitaiza' feki zawekwa hadharani

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA YATAMBA MERRIKH HAWATOKI** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimwapisha Nassor Ahmed Mazrui kuwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Ikulu jijini Zanzibar jana. Habari Uk. 5. **PICHA: IKULU**

# Kupiga nyungu rasmi Muhimbili

**Na Romana Mallya**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imeanza rasmi kutoa huduma ya kujifukiza, maarufu kupiga nyungu ili kukabiliana na maradhi.

Vilevile, hospitali hiyo ya kibingwa imebainisha kuwa wagonjwa wa matatizo ya kupumua wamepungua hospitalini hapo kwa sasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Prof. Lawrence Museru, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akizindua mashine ya kutoa dawa kwa njia ya mvuke ili kusaidia wagonjwa kupata tiba ya mfumo wa upumuaji kwa kutumia dawa ya Bupiji iliyoidhinishwa na serikali.

Alisema hospitali imezifunga mashine nne kwa ajili ya kujifukiza na kila moja imenunuliwa kwa Sh. milioni 7.5.

Alisema mashine hizo zimetengenezwa na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) na kwamba lengo la kuzifunga ni kuunga mkono jitihada za serikali za kukabiliana na magonjwa yanayohusiana na mfumo wa upumuaji.

Alisema mashine hiyo ina uwezo wa kuingiza watu sita kwa wakati mmoja ili kujifukiza.

"Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilielekeza kuimarishwa matumizi ya dawa za tiba asili na tiba mbadala kwa wagonjwa walioko hospitalini kama nyongeza kwenye tiba za kibingwa wanazopewa," alisema.

Prof. Museru alisema katika kutekeleza hilo, hospitali imekuja na utaratibu wa kuwaruhusu wagonjwa kwa hiari yao kutumia dawa za tiba asili za kunywa na mvuke (steam therapy) zilizoidhinishwa na serikali sambamba na tiba za kibingwa wanazopewa.

Pia alisema hatua ya ufungwaji wa mashine hizo itakwenda sambamba na kutoa fursa kwa wataalamu wa Muhimbili kufanya utafiti kubaini ufanisi wa baadhi ya dawa zinazogunduliwa na baadhi ya wataalamu wa tiba asili nchini, ili hatimaye waje na majawabu.

Alisema mashine tatu zimefungwa Upanga na moja imefungwa Mloganzila na zinaanza kutumika rasmi kuanzia leo kwa utaratibu maalum ambapo wagonjwa watakaoruhusiwa ni wale watakaokubali kwa hiari yao wenyewe.

Alisema huduma hiyo inatolewa kwa wagonjwa ambao wana uwezo wa kutembea na kusimama wenyewe kwenye mashine kwa muda usiozidi dakika tano.

Prof. Museru alisema huduma hiyo iko wazi kwa wananchi watakaopenda na kila mwenye uhitaji atatakiwa kuchangia Sh. 5,000.

Kuhusu wagonjwa wenye matatizo ya kupumua, alisema kwa sasa wamepungua, lakini hakutaja idadi yao ya awali na ya sasa.

"Kwa sasa idadi imepungua, tunawapokea wenye matatizo hayo lakini idadi imepungua na siyo kama walivyokuwa wanaandika kwamba tumezidiwa, waliokuja walipata tiba lakini tunaona idadi imepungua.

Mratibu wa Tiba Asili na Tiba Mbadala wa Mikoa na Wilaya kutoka Wizara ya Afya, Dk. Vumilia Liggyle, amepongeza hatua ya Muhimbili kufunga mashine za kutoa tiba mvuke na ametoa wito kwa hospitali na taasisi nyingine nchini kuiga mfano huo ili kuendelea kupambana na magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

Mzalishaji wa mafuta tete ya Bupiji, George Buchafwe, alisema wapo kwenye utafiti wa kupata dawa ya kusaidia magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza na wameitengeneza dawa hiyo na mashine hizo za kujifukiza.

Alisema ndiyo maana wapo katika Hospitali ya Muhimbili na kupitia njia hiyo ya kujifukiza itasaidia kupata majibu sahihi na ya uhakika.

"Utafiti upo lakini kwa sasa hatuwezi kusema chochote ndiyo maana tumeona twende na jambo moja moja, baada ya hapo tutakwenda na la pili.

# Adaiwa kujinyonga akitumia chandarua

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MKAZI wa Kijiji cha Kanazi, Kata ya Ntatumbila wilayani Nkasi mkoani Rukwa, Deus Kakusu (52), anadaiwa kujinyonga hadi kufa akitumia chandarua kutokana na kile kinachodaiwa ugumu wa maisha.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana wakati mke wake na watoto wake wakiwa wamelala.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kanazi, John Kaberaga, alisema kuwa ilipofika asubuhi ya siku ya jana, mke wa marehemu aliamka na kuanza kumwita mume akidhani yuko nje.

Baada ya mama huyo kutosikia mumewe akimwitikia, alidhani ameamka mapema kwenda shamba, hivyo alikwenda jikoni ili awashe moto kwa ajili ya kuandaa chakula cha siku hiyo, lakini aliposukuma mlango kuingia jikoni, aliona mwili wa mume wake ukiwa unaning'inia kwenye kamba.

Mwenyekiti Kaberaga alisema mama huyo alianza kupiga kelele huku akiangua kilio na majirani walifika na kukuta Kakusu amekwishafariki dunia.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Given Kisantola, alidai Kakusu hakuacha ujumbe wowote, lakini inadhaniwa alijinyonga kutokana na ugumu wa maisha kwa kuwa mara kwa mara alikuwa akilalamikia ugumu wa maisha na pia alionekana kukata tamaa na kuwa mlevi kupindukia.

Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Said Mtanda, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kutoa wito kwa wakazi wa wilaya hiyo kutokukaa kimya pindi wanapopitia kwenye matatizo mbalimbali ya kimaisha.

Alisema watu wengi wasioshirikisha ndugu zao au viongozi wa dini, wamekuwa wakifanya uamuzi usio sahihi, ikiwamo kujinyonga.

# Mbinu za kubaini 'sanitaiza' feki zaelezwa

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imebainisha mbinu kutambua vitakasa mikono (sanitizer) ambavyo siyo salama kwa matumizi.

Imesema mbinu hizo zinajumuisha muda wa kuyeyuka kwa vitakasa mikono hivyo, ikibainisha kuwa vile ambavyo baada ya kupaka hutumia zaidi ya dakika moja kuyeyuka, siyo salama kiafya.

Kwa mujibu wa TMDA, vitakasa mikono vilivyo salama huyeyuka kuanzia sekunde 30 hadi dakika moja mara baada ya kuwekwa mikononi.

"Kama sanitizer yako ukiweka mikononi inachelewa kuyeyuka zaidi ya dakika moja na ukiipaka inakuwa kama unapaka mafuta ya kawaida, ni wazi kuwa haiui vyema vijidudu au bakteria, kwa hiyo siyo salama," alisema Gerald Sambu.

Ofisa Uchunguzi wa Bidhaa wa Maabara wa TMDA, alibainisha hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maabara ya kuchunguza na kuhakiki ubora wa vitakasa mikono.

Alisema ubora unaotakiwa kwa matumizi ni kuanzia yenye alcohol 60 hadi 80 na yenye kiasi cha tindikali (acid) na nyongo (base/PH) kati ya sita hadi nane.

Alisema kama aina za vitakasa mikono vinavyotumiwa vipo chini ya viwango vilichowekwa, ni wazi kuwa haiwezi kuua vijidudu vinavyosambaza maradhi kama corona.

Sambu pia alisema vitakasa mikono vyenye alcohol zaidi ya 90 hadi 100, vina madhara kwa mtumiaji kwa sababu alcohol iliyozidi inasababisha mtumiaji kuchubuka mikono na kusababisha vijidudu kupenya kwenye ngozi na kuingia ndani ya mwili.

Alisema vitakasa mikono vingine visivyo na ubora ni vilivyozidi kiwango cha Glyceline na ukipaka vinanata kama asali.

Alisema namna nyingine ya kuvitambua visivyo salama, ni kutosajiliwa na kuwa na nembo inayomtambulisha mtengenezaji.

"Ninawasihi watumiaji kuangalia kama bidhaa zimesajiliwa na muda wa kuisha kwa matumizi yake ili kujihakikishia usalama," alisema Sambu.

Ofisa Elimu na Habari Mwandamizi wa TMDA, James Ndege, alisema wamekuwa wakiweka orodha ya wajasiriamali na wadau waliosajili vitakasa mikono kwenye tovuti yao ili kutoa elimu kwa jamii.

Alisema wamekuwa wakifanya ukaguzi mbalimbali wa bidhaa zilizopo sokoni ili kujiridhisha na ubora wake.

"Jamii inapaswa kutoa taarifa kwa mamlaka wanapoona wanatumia bidhaa tofauti na ubora uliothibitishwa na TMDA kwa kupiga namba ya bure ya 0800110084 na kuwasilisha malalamiko yao, na sisi tutayafanyia kazi haraka," alisema Ndege.

TMDA inatoa elimu hiyo wakati ambao dunia inapambana na virusi aina ya corona ambavyo vinaambukizwa kwa njia ya kushikana mikono na kuvuta hewa.

Njia mojawapo ya kudhibiti maambukizi ya virusi hivyo ni kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono vyenye alcohol ambavyo vinaua bakteria.

# Operesheni ondoa wamiliki hewa ardhi yaanza Julai mosi

**Na Munir Shemweta,**
ILEMELA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema kuanzia Julai mosi, mwaka huu, wizara yake itaanza uhakiki kitaifa kuwatambua na kuwaondoa wamiliki wote hewa wa viwanja nchini.

Lukuvi alisema hayo kwa nyakati tofauti jana katika ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela alipopokea taarifa ya utekelezaji majukumu ya sekta ya ardhi na eneo la Kigoto, Kata ya Kirumba alipogawa ankara za malipo kufuatia kuhitimishwa kwa mgogoro kati ya wananchi wa eneo hilo na Jeshi la Polisi akiwa kwenye ziara ya kikazi katika Mkoa wa Mwanza.

"Lazima tufanye uhakiki wa wamiliki wote wa ardhi ili kuwatambua na kuondoa wamiliki hewa, katika miji kuna maeneo mengi hayajengeki kwa sababu wamemilikishwa watu ambao hawapo," alisema Lukuvi.

Alisema, katika zoezi hilo halmashauri za wilaya zitatakiwa kuandaa jedwari la kumbukumbu za wamiliki ili uhakiki utakapoanza taarifa mpya zitakazojumuisha kumbukumbu zilizopo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), namba za simu pamoja na taarifa za kibenki zingizwe.

Lukuvi alisema, wapo wananchi waliojenga katika maeneo mbalimbali majina yanatofautiana na wengine majina ya kubuni, lakini hawapo Tanzania na kusisitiza kuwa ikibainika viwanja vyao vitapigwa mnada na aliwaonya watumishi wa sekta ya ardhi kutoharibu nyaraka kutokana na kuhusika kwao kwa namna moja ama nyingine katika umilikishaji.

Kwa mujibu wa Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi zoezi la kutambua wamiliki wa ardhi hewa halina lengo la kunyang'anya viwanja bali ni kujua wamiliki halali na kusisitiza kuwa watendaji wa sekta ya ardhi lazima wafanye zoezi hilo kwa umakini na uaminifu mkubwa.

"Najua baada ya kutangaza zoezi hili la uhakiki baadhi ya maofisa ardhi wataanza kuhangaika kuuza viwanja na wengine kunyofoa nyaraka, tumieni njia sahihi maana kila mtu ana haki ya kumiliki kiwanja zaidi ya kimoja cha msingi ni kufuata sheria," alisema.

Katika hatua nyingine Waziri Lukuvi aliwapatia ankara za malipo ya ardhi wananchi 600 wa eneo la Kigoto, Kata ya Kirumba katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela lililokuwa na mgogoro wa muda mrefu kati ya wananchi wa eneo hilo na Jeshi la Polisi.

"Wananchi wa Kigoto wamepatiwa eneo hili na Mheshimiwa Rais John Magufuli bila kutozwa gharama za thamani ya ardhi na ndio ninyi pekee katika Mkoa wa Mwanza mliopata eneo kwa gharama nafuu, mmwombee Rais Magufuli kwa kuwapatia eneo," alisema Lukuvi.

Vilevile, alitangaza kuanza awamu ya pili ya mpango wa 'Funguka kwa Waziri' utakaowezesha wananchi wenye migogoro ya ardhi kujaza fomu maalum na kuiwasilisha ofisi za ardhi za mikoa kwa ajili ya kutafutiwa ufumbuzi na waziri.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ilemela, aliwahakikishia wananchi wake kuwa serikali itahakikisha inamaliza migogoro yote ya ardhi katika Mkoa wa Mwanza kama ilivyoshughulikiwa mgogoro wa Kigoto katika kata ya Kirumba, Mkoa wa Mwanza.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mwanza, Eliah Kamyanda, alisema mgogoro wa eneo hilo ulidumu kwa takriban miaka 30 mpaka Rais aliporidhia wananchi hao kurejeshewa eneo hilo. Alisema, mgogoro huo ulipitia hatua mbalimbali na kwa sasa kazi ya upimaji imekamilika na wananchi wapatao 600 wamepatiwa ankara za malipo ya kumilikishwa.

## Waziri Mkuu aridhishwa kasi kupambana na nzige

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema ameridhishwa na kazi kubwa ya kupambana na makundi ya nzige yaliyovamia nchini iliyofanywa na Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na mashirika mawili ya kupambana na nzige barani Afrika.

Kazi hiyo inafanywa na Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani la Afrika Mashariki (Desert Locust Control Organization for Eastern Africa-DLCO EA) na Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu la Kusini na Kati mwa Afrika (International Red Locust Control Organization for Central and Southern Africa-IRLCO CSA).

Waziri Mkuu alisema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Engaruka, wilayani Monduli mkoani Arusha, baada ya kukagua shughuli ya udhibiti wa nzige katika kata ya Engaruka. Alisema ameridhishwa na kazi nzuri ya kupambana na nzige iliyofanyika tangu makundi hayo yalipoingia nchini, na kusisitiza licha ya kazi nzuri iliyofanyika ni muhimu kwa Wizara ya Kilimo ikaweka mikakati ya kukabiliana na makundi hayo yatakapoingia tena.

"Lazima tuwateketeze, nzige ni hatari na hawapaswi kupewa nafasi hata ya dakika moja kuingia kwenye mashamba yetu. Nzige hawa wana uwezo wa kusafiri umbali wa kilomita 200 kwa siku na kuteketeza zaidi ya hekta mbili kwa siku, hivyo ni lazima tuwateketeze."

"Muhimu zaidi ni kujipanga vizuri kukabiliana nao, ni lazima tuendeleze kazi nzuri tuliyoianza. Hawa wadudu ni hatari na wanazaliana mno. Ukimwona, kawaida anakuwa na rangi nyekundu, lakini ukimwona ana rangi ya njano huyo amebeba mayai tuwatekeze ili wasizaliane."

"Watanzania na Wana-Engaruka tuendelee kutoa taarifa na kujitokeza kwa wingi kushirikiana na wataalamu wetu kuteketeza makundi hayo."

Kwa upande wake, Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alisema kundi lililoendа Simanjiro limeshateketezwa, Siha wameshateketezwa na sasa hakuna nzige, Wilaya ya Mwanga ambako walikuwa wapite kuelekea Simanjiro nako kwa sasa hakuna nzige. "Tuliamua kupiga kambi hapa Engaruka ambako kulikuwa na makundi matatu makubwa jana na leo asubuhi ndege ya Shirika la Kupambana na Nzige wa Jangwani ambalo sisi ni wanachama, lilishambulia makundi hayo na helikopta ya kupambana na nzige wekundu nayo ilipulizia dawa pamoja na vijana waliokuwa wakipuliza." Prof. Mkenda amesema wataendelea kufuatilia maeneo ambayo nzige wametua na kuangalia kama wametaga mayai ili wayateketeze.

## Waya ulivyokatisha maisha ya bodaboda

**Na Gideon Mwakanosya,**
NAMTUMBO

DEREVA wa pikipiki katika Kijiji cha Mgombasi wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma, Kaimu Kinokwite (28), amefariki dunia kwa kukatwa shingo na waya wa umeme baada ya kunaswa na waya uliokuwa umekatisha barabarani.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo akiwamo Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mgombasi, Hance Mwailima, kijana huyo alionekana akirushwa kutoka katika pikipiki na kutupwa mbali baada ya kunaswa na waya huo.

Mwalimu Mwailima alidai kijana huyo alikuwa amebeba abiria wakitokea madukani kwenda Kijiji cha Mtumbatimaji na walipofika katika Kitongoji cha Dodoma jirani na shule hiyo, walipatwa na mkasa huo na kwamba abiria wake alikimbia baada ya tukio hilo.

Mwalimu huyo alidai katika eneo hilo la tukio hakukuwa na alama yoyote iliyokuwa kuashiria kuna kazi ya kuweka nyaya za umeme katika nguzo.

Kaimu Mtendaji wa Kijiji cha Mgombasi, Saidina Sandali, alikiri kutokea kwa tukio hilo huku Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mgombasi, David Kitalika, akiwataka madereva wa pikipiki kuwa waangalifu muda wote wakiwa barabarani hasa katika kipindi hiki cha utengenezaji na uwekaji nyaya za umeme katika vijiji vya Kata ya Mgombasi.

Mwili wa Kaimu ulizikwa jana katika makaburi ya Minazini, Kata ya Rwinga, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namtumbo wanakoishi wazazi wake.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE**

# TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**23/02/2021**

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kitauza gari chakavu kwa njia ya mnada wa hadhara mnamo tarehe 12/03/2021 siku ya Ijumaa.

Maelezo ya gari husika yameainishwa hapa chini:-

| GARI NAMBA | AINA/MODEL | MWAKA | AINA YA BODI | CC | CHASIS | INJINI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| SU38377 | NISSAN PATROL | 2010 | WAGON | 4169 | JNITCSY61Z05 | TD42212456 |

**Masharti ya mnada:-**

i. Chombo kitauzwa kama kilivyo mahali kilipo.
ii. Mnunuzi atalazimika kulipa papo hapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya chombo / kifaa alichonunua na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa gari husika na amana aliyolipia haitarudishwa.
iii. Mnunuzi atatakiwa kuondoa au kuchukua chombo alichonunua katika muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
iv. Ruhusa ya kuangalia vyombo itatolea siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
v. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi katika eneo kilipo chombo.

**Dkt. Godwin E. Kaganda**
**NAIBU MKUU WA CHUO - MIPANGO, FEDHA NA UTAWALA**

# Waziri Jafo awapa somo wanaume wasiotahiriwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amewataka wanaume ambao hawajafanyiwa tohara, kuchangamkia huduma hiyo ili kuepuka kupata magonjwa mbalimbali ikiwamo saratani.

Vilevile, amewaagiza makatibu tawala wa mikoa kufuatilia ununuzi wa dawa na kuhakiki matumizi yake kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Jafo alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipozindua magari maalum kwa ajili ya utoaji huduma tembezi ya tohara kinga kwa wanaume kwenye mikoa ya Mara, Mwanza, Shinyanga na Simiyu.

Magari hayo matatu yamegharimu Sh. bilioni 1.2 kwa ufadhili wa watu wa Marekani kupitia Mfuko wa Rais wa Marekani wa kupambana na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (PEPFAR) na Kituo cha Kimataifa cha Kujikinga na Maradhi (CDC) kwa kushirikiana na wadau wa IntraHealth International.

Akizindua magari hayo, Jafo alisema mwanaume ambaye hajafanyiwa tohara ana nafasi kubwa ya kupata magonjwa ya zinaa na saratani.

"Wataalamu na watafiti wanasema mwanaume aliyetahiriwa, inasaidia kujikinga na maambukizi ya VVU kwa asilimia 60," alisema.

Aliwahimiza wanaume hao kujitokeza kufanyiwa tohara huku akiagiza utuzanji wa magari na vifaa vilivyomo ndani yake, ili kutoa huduma stahiki kwa wananchi.

"Ninaomba nipate orodha ya vitu vyote vilivyomo, ninataka nikifanya ziara ya kikazi katika mikoa hiyo, pia nitakagua kama vifaa vipo, sitaki kusikia vifaa vimetolewa na kupelekwa kwenye hospitali binafsi au vimeuzwa," alionya.

Alishukuru Shirika la Intra Health International na CDC kwa kutoa magari hayo ambayo yatasaidia kutoa huduma kwa wananchi ambapo taarifa zinaonyesha kuwa kati ya mikoa 26 ya Tanzania Bara, 19 inakabiliwa na tatizo la maambukizi ya Ukimwi ikiambatana na watu kukosa tohara.Kuhusu upatikanaji wa dawa, Jafo alisema serikali hivi karibu ilitoa Sh. bilioni 93.3 ambazo zimepelekwa kwenye hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati kwa ajili mambo mbalimbali ikiwamo dawa.

Alisema kati ya hizo, Sh. bilioni 41.3 zimepelekwa Bohari ya Dawa (MSD) na Sh. bilioni 52 zimepelekwa kwenye vituo vya afya, asilimia 35 ya fedha hizo ambayo ni Sh. bilioni 18 ni kwa ajili ya dawa.

"Makatibu tawala wa mikoa nendeni mkafuatilie ununuzi wa dawa, fanyeni ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha dawa zinapatikana, sitaki kusikia hakuna dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya wakati serikali imetoa fedha," aliagiza.

Alisisitiza waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha wanatumia mifumo ya kielektroniki ya uendeshaji shughuli za afya na mifumo ya matumizi ya fedha katika vituo hivyo. Awali, Mkurugenzi Mkazi wa Intra Health International, Dk. Lucy Mphuru, alisema taasisi hiyo inafanya kazi nchini kwa miaka 20 hivi sasa na kwa miaka 10 imekuwa ikishughulika na masuala hayo ya tohara ili kupambana na maambukizi ya VVU.

Alisema magari hiyo ni ya kisasa ambapo kuna chumba cha upasuaji mdogo, vitanda vitatu na vifaa tiba vya dharura na kila moja limegharimu Sh. milioni 400.

"Magari haya yametolewa ili kuhakikisha huduma ya tohara kwa wanaume wakubwa inafanyika na kuwafikia walio pembezoni ikiwa ni njia ya kupunguza maambukizi mapya ya Ukimwi na huduma hiyo ni bure," alisema.

Alibainisha kuwa tangu kuanza kampeni hiyo katika mikoa hiyo minne, wanaume milioni 1.82 wamefanyiwa tohara.

Awali, Mkurugenzi wa Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa TAMISEMI, Dk. Ntuli Kapologwe, alisema serikali imefanya uwekezaji mkubwa wa ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma vinavyogharimu Sh. bilioni 68 ili kusaidia kutoa huduma ya tohara.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, Gerald Mweli, alisema serikali imewekeza kwa kiwango kikubwa kwenye kuboresha huduma za afya, ununuzi wa vifaa tiba na kuajiri watumishi.

# Wakili A. Kusini aunga jitihada za JPM kupambana corona

**Na Maulid Mmbaga**

MJUMBE wa Baraza la Mawakili kutoka Afrika Kusini, Sibelo Sibanda, ameunga mkono jitihada za Rais John Magufuli, za kupambana na virusi vya corona na kutoa wito kwa Afrika kuwa makini dhidi ya tahadhari za Covid-19.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Sibanda alisema Serikali ya Tanzania imewahimiza wananchi wake kutumia zaidi dawa za asili kulikabili janga la corona kuliko zinazotoka nje jambo ambalo linawaweka katika hali ya usalama zaidi.

Alisema anaunga mkono hatua za Rais Magufuli kutowaweka wananchi karantini kwa kuwa kufanya hivyo inamweka mtu katika hatari zaidi ya kupata magonjwa ya milipuko kwasababu mtu anapokaa ndani kwa muda mrefu kinga za mwilini zinapoteza uwezo wa kupambana na maradhi.

"Alichokifanya Rais Magufuli kinafaida kwa Afrika nzima na mimi nipohapa leo (jana) kwa kuwa ni miongoni mwa Afrika na baadhi ya sehemu ambazo wametoa agizo la kukaa karantini ndizo zinaongoza kwa watu kupoteza maisha.

"Pia nina wahimiza watu Afrika kwa ujumla kuwa makini na tahadhari wanazozichukua dhidi ya corona na wajikite zaidi katika kutumia dawa asilia na kama Afrika tunapaswa kufanya kila jitihada kuhakikisha tunapata suluhu ya moja kwa moja dhidi ya janga hili," alisema.

Alisema kuwa kwa mujibu wa taarifa ya uvaaji wa barakoa hauna uthibitisho wa kujitosheleza kuwa unamkinga mtu dhidi ya corona, na kusisitiza hatua ya Rais Magufuli ya kutaka wananchi wake kuwa watumie za ndani kuliko za nje ni sahihi kwa kuwa zinazotoka nje hazina uhakika wa usalama.

Alisema Rais Magufuli alichukua hatua nyingi za kimaendeleo ambazo zimekuwa na manufaa makubwa katika nchi kwa ujumla na hiyo ilitokana na hatua ya kutowaamuru watu kukaa ndani hali iliyowawezesha kuendelea za kulijenga taifa tofauti na sehemu nyingine.

"Tukiwa kama wakereketwa wa kutetea maslahi ya Waafrika tumefurahishwa na wananchi wa Tanzania kukubali kufuata maelekezo waliyopatiwa na kiongozi wao na wanapaswa kujivunia kwa hatua hiyo kwani imewasaidia, hivyo tunapaswa kusimama imara na tujilinde wenyewe," alisisitiza.



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga (wa pili kulia), akibadilishana mikataba ya makubaliano na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, jijini Dar es Salaam jana, baada ya Benki Kuu kuamua mali na madeni ya Benki ya China Commercial, kuhamishia NMB, kwa kwa mujibu wa sheria. Kulia ni Naibu Gavana Udhibiti wa Ndani na Utawala, Julian Banzi Raphael na Mkuu wa Idara ya Sheria wa Benki ya NMB, Lilian Komwihangire. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Madeni, mali za Benki ya China zahamishiwa NMB

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu ya Tanzania(BoT), imesema mali na madeni yote ya China Commercial Bank Limited, vitachukuliwa na Benki ya NMB Plc.

Uamuzi huo ulitangazwa jana na Gavana wa BoT, Prof. Florens Luoga, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Alisema BoT, NMB na wadau wengine wanaendelea kuandaa taratibu za kisheria za kukamilisha mchakato wa uhamishaji wa mali na madei ya benki hiyo.

Aidha, alisema wateja wenye mikopo wanatakiwa kuendelea kulipa mikopo kulingana na mikataba yao, na kwamba maslahi ya wateja wenye amana yatalindwa ili kuleta utulivu na uhimilivu katika sekta ya fedha.

Kwa mujibu wa Prof. Luoga, wateja wenye amana na wadai wengine wa China Commercial Bank watataarifiwa tarehe ya kuanza kupata huduma za kibenki kupitia NMB. "Katika kusimamia sekta ya fedha na mamlaka ya kisheria Novemba 19, mwaka 2020, BoT iliamua kuiweka China Commercial Bank Limited chini ya usimamizi wake, baada ya kubainia ina upungufu wa mtaji kinyume cha matakwa ya kisheria," alifafanua.

Aidha, alisema benki hiyo ilipewa leseni na kuanza shughuli za kibenki nchini mwaka 2015, na kuwa miongoni mwa benki zenye ukuaji wa chini uliosababisha hasara kwenye biashara kwa kipindi chote toka kuanza kutoa huduma za kibenki hadi kuchukuliwa na BoT ilikuwa na mali zisizozidi Sh. bilioni 5, na ilikuwa na tawi moja Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Prof. Luoga, BoT ilifanya jitihada kupitia wamiliki, Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Benki kuwataka kuongeza mtaji kufikia kiwango kinachohitajika kisheria, na kwamba pamoja na kupewa muda wa kutosha hawakufanya hivyo. "Baada ya kuweka chini ya usimamizi wake, BoT ilisitisha utoaji wa huduma za kibenki kwa benki hiyo kwa siku 90 ili kuipa nafasi BoT kutathmini hatua za kuchukua ili kupata ufumbuzi," alisema.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema ndani ya siku 60 watakuwa wamekamilisha taratibu zote na wateja watapata huduma zote muhimu za kibenki katika matawi 227 yaliyopo nchini.

"Kinachofanyika sasa ni kuwajua wateja wa iliyokuwa China Commercial Bank, kwa kuchambua majina na taarifa zote muhimu. Wale wateja waliokuwa na mikopo waendelee kurejesha, waje katika matawi yetu ya Bank House na Ohio watapata maelezo yote muhimu," alisema.

HABARI KITAIFA



Mafundi wa wakiendelea na ujenzi wa kingo za Mto Ng'ombe, eneo Shekilango, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana, awali ulikuwa ukielemewa na mafuriko nyakati za mvua na maji kuleta madhara kwenye makazi ya watu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mawaziri wapya Zanzibar waahidi makubwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAWAZIRI watatu walioteuliwa, jana waliapishwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, huku wakiahidi makubwa.

Walioapishwa ni Saada Mkuya Salim, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais; Omar Said Shaaban (Biashara na Maendeleo ya Viwanda) na Nassor Ahmed Mazrui (Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto).

Rais Dk. Mwinyi pia alimwapisha Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Salum Yussuf Ali, aliyemteua Februari 10, mwaka huu.

Wakizungumza baada ya kula kiapo cha utii na uaminifu, mawaziri hao walisema watafanya kazi kwa ufanisi ili kumsaidia Rais kuwaletea maendeleo wananchi.

Omar Shaaban alisema amejipanga kuhakikisha anaifanyia kazi changamoto ya wafanyabiashara wa Zanzibar kupeleka biashara zao katika soko la Tanzania Bara.

Alisema pamoja na jitihada mbalimbali zilizochukuliwa katika kutatua changamoto hiyo, lakini atakaa na kuona wapi wenzake waliopita wamefikia ili kulichukulia hatua za haraka.

"Nitakaa na wenzangu ili tujue lipi lililokwama na nini kilichokwamisha kwa kuzitambua changamoto ili ziweze kuondoka kama Rais anavyosema mara kwa mara," alisema na kuongeza:

"Hakutakiwi kuwa na vikwanzo katika ufanyaji wa biashara na kama tunavyojua Zanzibar ni kitovu cha biashara na lazima irudi katika hadhi yake."

Waziri Omar alisema suala la uanzishwaji wa viwanda Zanzibar limekuja wakati mzuri kutokana na Rais wa Zanzibar kuasisi sera yake ya uchumi wa bluu unaoendana na malighafi inayotokana na bahari kurasimishwa, hivyo anaamini viwanda vitakuwa na msukumo wa kipekee kutokana na uono wa Rais kuhakikisha uchumi wa Zanzibar unakuwa na Zanzibar inanufaika na malighafi zilizopo kwenye bahari.

Naye Waziri Ahmed Mazrui alisema anafahamu kuwa wizara yake ina changamoto nyingi, lakini amejiandaa kwenda kufanya kazi.

Alisema ana wajibu wa kuonyesha na kuthibitisha dhamira ya chama chake (ACT-Wazalendo) kuhusu maridhiano ya kisiasa na wamejiunga katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK)) katika kuijenga serikali hiyo.

Aidha, alisema anaamini kwamba kutokana na mipango iliyopo chini ya usimamizi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, wamejipanga katika kutekeleza masuala ya kutoa huduma kwa wananchi.

Naye Waziri Saada Mkuya alisema wananchi wa Zanzibar watarajie mambo makubwa katika ofisi anayoiongoza ambayo inashughulikia mambo mbalimbali yaikiwamo masuala ya Ukimwi, mazingira, dawa za kulevya na walemavu.

Aidha, alisema katika kueleekea uchumi wa bluu, ni lazima kutekeleza uchumi endelevu kwa kuhakikisha wanasimamia kwa umakini mkubwa mazingira.

Akizungumzia changamoto ya vijana wanaotumia dawa za kulevya, Mkuya alisema Wizara kupitia Kamisheni itahakikisha inakidhi mahitaji ya sasa katika kuwaokoa vijana hao ambao ni nguvu kazi ya Taifa.

Alisema masuala ya mazingira na ulemavu ni lazima sera na sheria zote zinazotungwa na utekelezaji wa mipango kazi ya taasisi, wizara na mashirika kuhakikisha yanazingatia masuala yote mtambuka.

# Kamati za Bunge kuanza vikao Jumatatu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

VIKAO vya Kamati za Kudumu za Bunge vinatarajiwa kuanza Machi 8, mwaka huu, kwa ajili ya mkutano wa Bunge la Bajeti uliopangwa kuanza Machi 30, mwaka huu.

Miongoni mwa shughuli za kamati, wabunge watapokea mapendekezo ya serikali kuhusu mpango, kiwango na ukomo wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2021/22.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, Ofisi ya Bunge, kamati hizo zitahitimisha shughuli zake Machi 26, mwaka huu, huku ikibainisha kuwa ukomo huo utatolewa kwa wabunge kwa masharti ya Kanuni ya 116(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020.

Kanuni hiyo, inasema: 'Tarehe kumi na moja ya mwezi Machi ya kila mwaka au tarehe ya siku nyingine ya kazi inayofuata iwapo tarehe hiyo itakuwa si siku ya kazi, Waziri anayehusika na masuala ya mipango atawasilisha kwa wabunge, mapendekezo ya Serikali ya mpango kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Pia siku hiyo, Waziri anayehusika na masuala ya fedha, atawasilisha kwa wabunge, mapendekezo ya Serikali ya kiwango cha ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Pia shughuli zingine za kamati ni kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Aidha, taarifa hiyo inaonyesha kuwa kamati hizo za kisekta zitafanya ziara ya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali Kuu na Taasisi za Umma.

Kadhalika, kuchambua taarifa za uwekezaji uliofanywa na serikali kupitia mashirika, taasisi na kampuni ambazo serikali ina hisa na kukagua shughuli za uwekezaji zilizofanywa na serikali.

Pia kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Katika vikao hivyo, kutakuwa na uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa pili wa Bunge la 12.

Taarifa hiyo, inabainisha kuwa kutakuwa na mashauriano kati ya Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti kuhusu masuala muhimu yatakayojitokeza kwenye kamati za kisekta wakati wa kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti mwaka 2019/20 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2020/21.

# Hukumu ya mwekezaji kesi kulima dawa za kulevya Machi 26

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HATIMA ya mwekezaji wa kigeni kutoka nchini Poland, Damian Jankowski na Watanzania watatu wanaokabiliwa na kesi ya ulimaji wa dawa za kulevya na kufanya mauzo ndani na nje ya Tanzania, kujulikana Machi 26, mwaka huu.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Moshi, Bernazitha Maziku, anayesikiliza kesi hiyo namba 79 ya mwaka 2020, anatarajiwa kusoma hukumu yake.

Jana, Hakimu Maziku aliiambia mahakama hiyo kuwa: "Kazi ya kusikiliza maelezo ya upande wa mashtaka, ushahidi wa mashtaka na utetezi wa washtakiwa umekamilika na kinachofuata ni hukumu."

Jankowski na wenzake ambao ni mkewe Eliwaza Pyuza, mfanyabiashara Hanif Kanani na Boniface Kessy, wanakabiliwa na makosa manne ya kulima bangi ya kisasa miche 729, kujihusisha na matumizi ya bangi, kufanya mauzo na kusafirisha bangi kwenda ng'ambo.

Februari 17, mwaka huu, mahakama hiyo ilimuona Jankowski na washtakiwa wenzake watatu ambao ni raia wa Tanzania, wana kesi ya kujibu katika mashtaka hayo baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi wa upande wa mashtaka.

Upande wa mashtaka, ukiongozwa na Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS), Ignas Mwinuka na Verdiana Mlenza, ulifunga ushahidi wake, baada ya mashahidi 11 kutoa ushahidi wao pamoja na kuwasilisha vielelezo 36.

Washtakiwa hao katika hati ya mashtaka wanakabiliwa na mashtaka manne ambayo ni kulima dawa za kulevya kinyume na kifungu cha 11 (1) (a) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 5 ya Mwaka 2015.

Mshtakiwa wa kwanza, pili na wa tatu wote kwa pamoja wanadaiwa kuwa Februari 8, mwaka jana, katika eneo la Njia Panda ya Himo, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, walikutwa wamelima miche ya bangi 729.

Wakati kosa la pili ambalo linawakabili mshtakiwa wa kwanza, pili na wa tatu, ni kusafirisha bangi kinyume na kifungu cha 15A (1) (2) (C) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 15 ya Mwaka 2017 kama ilivyofanyiwa marejeo.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washtakiwa hao pia wanadaiwa kukutwa na kilogramu 15.6 za bangi katika eneo la Shirimatunda, Manispaa ya Moshi, Februari 8, mwaka jana. Kosa la tatu ni kusafirisha dawa za kulevya kinyume na kifungu cha 15A (1) (2) (C) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 5 ya Mwaka 2015 kama ilivyofanyiwa marejeo kifungu cha 9 cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 15 ya mwaka 2017.

Kosa la nne ni matumizi ya dawa za kulevya, kinyume na kifungu cha 18 (a) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 5 ya Mwaka 2015. Kesi hiyo itaendelea tena leo mahakamani hapo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kero za umeme, maji zishughulikiwe haraka

**TATIZO** la kukatika kwa umeme nchini limeendelea kukua na sasa linaleta madhara kwenye shughuli za uzalishaji zinazotegemea umeme, jambo ambalo ni kilio kwa wananchi.

Kwa sasa ni kawaida umeme kukatika bila taarifa yoyote kuwajulisha wananchi kuwa umeme katika eneo lao utakatika kuanzia muda fulani hadi fulani, badala yake imekuwa ya kushtukiza.

Umeme ni muhimu sana kwenye shughuli za uzalishaji na hutegemewa na wengi kupata ajira na kulipa kodi muhimu.

Kwa sasa kutokana na kutotabirika kwa umeme, wengi wamejikuta wanakwenda maeneo ya uzalishaji wakishindwa kufanya lolote, matokeo yake wanapoteza muda na nauli.

Hiyo yote ni kwa sababu hakuna taarifa muhimu kwa ajili ya wateja kwamba katika eneo fulani umeme utakatika kuanzia muda fulani hadi muda fulani, lakini kinachofanyika sasa ni kukata na kurudisha.

Kwa sasa baadhi ya maeneo kama Kariakoo matumizi ya majenereta yamerudi kama enzi za mgao wa umeme, huku gharama za uzalishaji zikiongezeka na bei ya bidhaa kupanda ili muuzaji apate faida aliyoitarajia na aweze kulipa kodi.

Licha ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kueleza kuwa kukatika kwa umeme kunasababishwa na matengenezo wanayoendelea nayo, lakini ni muhimu kutoa taarifa za mara kwa mara.

Kukatika kwa umeme kumekwenda sambamba na kukatika kwa maji kwenye maeneo mengi, jambo ambalo linawafanya wananchi kukosa huduma zote muhimu za maji na umeme.

Umeme na maji ni muhimu kwa maisha ya binadamu yeyote, na ni muhimu kwamba watu wakijua suala la umeme kukatika wataangalia aina ya vyakula watakavyohifadhi kwenye friji, ikiwa ni pamoja na kuchukua tahadhari ili visiharibike.

Baadhi ya viwanda vimeshindwa kuendelea na uzalishaji kutokana na umeme kukatika kwa muda mrefu na bila taarifa yoyote, jambo linalowafanya washindwe kumudu gharama za uzalishaji.

Kwa bidhaa zenye bei elekezi ni ngumu sana kupandisha bei licha ya kuzalisha kwa gharama kubwa, ni muhimu sana kuhakikisha umeme unapatikana, na kama ni matengenezo ni muhimu yakafanyika kwa haraka.


Waathirika wakubwa ni wajasiriamali wadogo ambao shughuli zao hazifanikiwi bila umeme, jambo ambalo litawarudisha nyuma kimaendeleo na wakati huo huo kodi iko pale pale.

Ni muhimu TANESCO kutoa taarifa za ratiba ya umeme kabla ya kukatwa, kwa kuwa inafahamika kuwa eneo fulani umeme utakatika kuanzia saa fulani hadi fulani, ili kila mtu apangilie ratiba zake, ikiwamo kuandaa mavazi kwa kupasi nguo mapema au kuwa na nishati mbadala ya kupikia.

Pia ni muhimu mamlaka za maji kutoa taarifa za mgao wa maji ili wananchi waweke akiba kuliko hali ilivyosasa ya huduma hiyo kukosekana kila wakati bila taarifa.

Taarifa zitasaidia watu kupanga ratiba zao na kupunguza usumbufu na hasara ambayo inaweza kuepukika, tunaona ni muhimu vitengo vya habari vya taasisi kuwa na mawasiliano na wateja wao kila mara hasa kunapokuwa na mabadiliko ya huduma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Magari haya ya taka yawe chachu usafi Dar es Salaam

**MKUU** wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, amepokea magari 20 na makontena 65 ya kuhifadhi taka, huku akiwahimiza wakazi wa mkoa wake kuhakikisha wanazingatia usafi wa mazingira.

Amewaelekeza wakurugenzi wa manispaa zote, kuhakikisha suala la usafi linapewa kipaumbele na magari hayo yatunzwe ili yadumu kwa muda mrefu, yakitatua kero ya usafi jijini humo.

Vilevile, wito wake kwa wananchi ni waepuke tabia ya kutupa taka kwenye mitaro na mito kwa kuwa kufanya hivyo kunasababisha kuziba mitaro na kwamba watakaohusika kuchafua mazingira, sheria itafuata mkondo wake kuwawajibisha.

Hapo nianze kwa kumpongeza Mkuu wa Mkoa kwa juhudi za kutaka kuhakikisha jiji na mkoa kwa ujumla unakuwa katika mazingira safi na ya kuvutia kwa bora.

Pia ni vyema kukumbushana mambo kadhaa ya msingi ambayo ninaamini kama yatazingatiwa, mkakati wake wa kutaka jiji la Dar es Salaam liwe safi, mtu anaweza kufanikiwa nalo.

Kwanza niseme, jiji linatambua kuwapo ongezeko la aina tofauti za taka ngumu, zikiwamo za majumbani, viwandani na hospitalini, zinazotupwa katika maeneo mbalimbali na kusababisha uchafuzi wa mazingira.

Aidha, jiji linakadiriwa kuzalisha zaidi ya tani 4,600 za taka kwa siku, huku kati ya hizo, asilimia 45 hadi 50 tu ndizo zinazopokelewa katika dampo, kutoka wastani wa tani 1,200 hadi 2,000 za taka zinazokisiwa kuzalishwa kila siku, Dar es Salaam.

Ni hatua inayoelezwa kwamba taka zinazobaki, huishia kwenye maeneo ya wazi, mitaro ya maji, barabara na makazi ya watu. Ni hali inayochangia kuchafua mazingira ya Dar es Salaam, hata kwingine kunakozalishwa.

Wakati hayo yanafanyika kuna uchafuzi mwingine wa mazingira unaofanywa na wafanyabiashara wadogo, ambao wamegeuza mitaro ya maji ya mvua kuwa sehemu ya kufanya shughuli zao.

Ni mtindo unaosababisha watupe taka katika mitaro hiyo, huko wakichafua mazingira na hata wakati inatokea mvua zinanyesha, maji yanasambaa mitaani kutokana na mitaro kuzibwa kwa taka.

Kimsingi, mkakati wa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ni mzuri, lakini unaweza kukabiliwa na tatizo hilo ambalo ni vyema angelitatua kwa kuwaondoa wafanyabiashara wote kwenye mitaro ya maji ya mvua.

Hivyo, Mkuu wa Mkoa anapotoa wito kwa kuepuka tabia ya kutupa taka kwenye mitaro na mito, ni vyema kumfahamisha kuwa wahusika wakuu wa kuchafua mazingira si watu waliopo nyumbani tu, bali na wadau wengine mitaani.

Biashara zao ni muhimu kwa mahitaji ya watu wengi. N vyema wakawa wa kwanza kuzingatia usafi na hasa kuondoka kwenye mitaro na kuiacha iwe wazi kwa ajili ya kupitisha maji ya mvua.

Vilevile, ni kwa muda mrefu kuna mtindo wa kukusanya taka kwenye makontena yanayojaa hadi kumwagika chini na kuachwa muda mrefu bila ya kuondolewa. Ni hali hatari kwa afya za umma.

Hivyo narejea, jiji letu kupata magari na makontena ya kutunzia taka, tunapaswa kuwa hatua ya mabadiliko, tukiachana na mazoea ya utupaji taka ovyo, bali igeuke kuwa kichocheo cha kukabili magonjwa ya milipuko kama vile kipindupindu, kuhara na kutapika.

Wakati tukiwa katika mikakati ya kuliweka jiji katika hali ya usafi, elimu kuhusu utunzaji wa mazingira inapaswa kutolewa kwa wingi. Uchafu jijini unachangiwa na watu kukosa elimu.

Watu wanapoelimishwe kuhusu usafi wa mazingira, wanapaswa kujua umuhimu wa kutii sheria zilizopo, pia usimamizi wa sheria za usafi wa mazingira upewe kipaumbele na wananchi wazingatie usafi bila shuruti.

HABARI KITAIFA

## Bil. 680/- kukarabati Reli ya Kati

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

SERIKALI kupitia Shirika la Reli Nchini (TRC) inatekeleza mradi wa uboreshaji wa Reli ya Kati kutoka Stesheni ya Dar es Salaam hadi Isaka mkoani Shinyanga umbali wa kilometa 970 kwa gharama ya Sh. bilioni 680.

Hatua hiyo inalenga kuhakikisha kunakuwapo na usafiri wa uhakika na kuaminika na kuongeza mwendokasi wa treni kutoka wastani wa sasa wa kilometa 35 mpaka 70 kwa saa.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Msimamizi wa Timu ya Ukarabati kwa kipande ya Isaka hadi Itigi, Bernard Mbonde kwa Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Tabora wakati wakikagua utekelezaji wa mradi huo.

Alisema mradi huo una jumla ya mikataba 71 ikiwamo minne ya ukarabati wa njia ya reli kuanzia Dar es Salaam hadi Isaka, ununuzi wa mabehewa 44, vichwa vitatu vikubwa, ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kisasa wa ishara ya mawasiliano wa kuongozea treni na mtambo wa marekebisho ya njia ya reli.

Mbonde alisema vichwa vitatu na mabehewa 44 yanatarajiwa kuwasili nchini wakati wowote mwezi huu ili kusaidia kuongeza ufanisi katika usafishaji wa mizigo na abiria.

Alisema sehemu ya pili ambayo ni kubwa iko mkoani Tabora, njia za reli zilizobadilishwa kwa kuondoa reli ndogo na kuweka nzito ni kilometa 45.5 ambayo ni kutoka Igalula hadi Tabora na kuongeza kuwa njia za reli zilizokarabatiwa ni kilometa 125 kutoka Itigi hadi Tabora.

Mbonde aliongeza kuwa njia za kumpuzikia treni zimerefushwa katika stesheni mbalimbali kutoka mita 400 hadi 600 ili kuwezesha treni ndefu kupumzika.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Tabora, Hassan Wakasuvi, alilitaka Shirika la Reli Tanzania kuhakikisha linarudhisha utaratibu wa zamani wa uendeshaji na usimamizi wa shirika hilo ikiwamo kufufua magenge ambayo yatasaidia kuimarisha ulinzi na usafishaji wa miundombinu.

Alisema kukosekana kwa watumishi wa reli katika magenge mengi, miundombinu ya reli iko hatarini kuhujumiwa na kuharibiwa na mifugo na wakulima wanaolima kandokando ya reli kwa kuwa hakuna mtu anayesimamia.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, aliwataka wawekezaji kwenda mkoani humo kuwekeza katika shughuli mbalimbali kwa kuwa kwa sasa njia ya reli iko vizuri na wanatarajia kuongeza mabehewa.

# Samia ataka mtoto wa kike awe kiongozi

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amesema serikali itaandaa mpango wa kitaifa wa kuwajengea ujasiri watoto wa kike tangu wakiwa shuleni ili kuja kuwa viongozi baadae.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika mkutano mkuu wa mwaka wa tatu wa wanawake katika uongozi ulioandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Mkutano huo ulikwenda sambamba na mahafali ya nne, tano na sita ya programu ya Mwanamke Kiongozi ambayo ilizinduliwa na Samia mwaka 2016 na mpaka sasa jumla ya wanawake 150 wamenufaika nayo na waliohitimu siku hiyo ni 60.

Samia alisema mpango huo unakusudia kumjengea mtoto wa kike ujasiri tangu akiwa na umri mdogo.

Mkutano huo ulibebwa na kauli mbiu isemayo, "Ukuzaji wa vipaji vya wanawake walio katika uongozi ili kuwa na mashirika endelevu."

Alisema uamuzi wa kubuni mpango huo unatokana na ukweli kwamba, Tanzania bado inahitaji wanawake zaidi katika nafasi za juu za uongozi ili kupiga hatua katika mipango yake mbalimbali ya maendeleo.

"Uchunguzi mbalimbali zimethibitisha kuwa wanawake wengi katika nafasi za juu za uongozi ndivyo kasi ya maendeleo inavyopatikana, tuna idadi ya wahitimu kutoka Programu za kuinua wanawake kwa baadae, hii inaweza kusaidia utekelezaji wa mpango wa ushauri kwa kuwaelimisha wasichana wadogo kile kinachohitajika wao kuwa viongozi wazuri, "alisema.

Samia alimtaka Waziri wa Nchi,Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu, Jenister Mhagama, kwenda kujipanga vizuri na kuona namna mpango huo unaweza kutekelezwa kwa kuwafikia wasichana wote katika Shule za Sekondari nchini kote.

"Tunapaswa kufikiria zaidi namna ya kusaidia watoto wa kike kuweza kujiamini na kuaminika na kufanya kazi zao na kutoa matokeo chanya," alisema.


Aliipongeza ATE kwa kufanikisha kuandaa mkutano huo ambao unakwenda sambamba na juhudi za serikali za kuhakikisha idadi ya wanawake katika nafasi za juu za uongozi inazidi kuongezeka.

Alisema kuna idadi kubwa ya wanawake katika bodi za wakurugenzi za kampuni mbalimbali.

"Mchango wa ATE katika kukuza na kuboresha uchumi wa taifa ni mkubwa, serikali inathamini na kutambua mchango huu na tumejipanga vizuri kuhakikisha tunafanya kazi kwa kushirikiano na wadau ili kuweza kufikia malengo ya Agenda ya Afrika ya mwaka 2063 ya Afrika tuitakayo yenye Maendeleo Endelevu na Ukuaji wa Uchumi Unayomshirikisha kila mtu," alisema.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa ATE, Dk. Aggrey Mlimuka, alisema utafiti unaonyesha taasisi zinazoongozwa na wanawake zina matokeo chanya, ongezeko la uzalishaji na ukuaji wa kiuchumi.

Alisema lengo la programu hiyo ya mwanamke, siyo kuwa na wawakilishi wanawake bali wawe wenye uwezo wa kujenga hoja na kuleta mabadiliko ndani ya taasisi wanazoziongoza na tayari wamepata matokeo chanya kwa wanufaika.




Mkurugenzi wa Teknolojia na Uendeshaji wa Benki ya TPB, Jema Msuya (katikati) na Mkurugenzi wa Airtel Money, Isack Nchunda, wakizindua huduma ya pamoja ya mawasiliano, baada ya kuingia ubia wa kushirikiana katika huduma za kifedha, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Biashara wa TPB, Deo Kwiyuka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Airtel, TPB waungana huduma fedha kidigitali

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Airtel Tanzania imeingia ubia na Benki ya TPB kuboresha na kupanua wigo wa huduma za kifedha nchini kupitia huduma ya Airtel Money.

Akiongea katika mkutano na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Airtel Money, Isack Nchunda, alisema; "Ubia tunaoingia hapa leo utasaidia sana kuboresha huduma tunazotoa kwa kuwafaidisha zaidi mawakala wetu wa Airtel Money waliopo kila mahali nchini mahali benki ya TPB imefika. Pia Wateja wa Airtel Money sasa watakuwa na uhakika kufanya miamala yao kwa uhakika wakiwa popote."

Nchunda alisema mawakala sasa hawatakuwa na haja ya kubeba bulungutu la fedha na kusafiri umbali mkubwa kupata salio kwa kuwa watahudumiwa kwenye tawi lolote la TPB karibu yake.

"Muunganiko wetu utaendelea kukamilisha dhamira yetu tuliyojiwekea sisi wabia ya kutoa huduma nafuu, kwa haraka, bila mipaka ili kukidhi mahitaji ya wateja wetu ya kila siku," alisisitiza Nchunda.

Akiongea kwa niaba ya TPB, Mkurugezi wa huduma za kimtandao, Jema Msuya, alisema wanaamini suluhisho la huduma za kifedha katika utoaji huduma unatija katika kuleta maendeleo ya kiuchumi.

"Benki ya TPB kila tuponakuja na huduma yenye ubunifu zaidi lengo letu ni kuongeza au kutoa suluhisho zaidi kwa wateja wetu pamoja na kuwapatia huduma kwa unafuu huku tukizingatia ubora zaidi. Ubia wetu na Airtel Money leo hii unadhihirisha dhamira yetu hiyo ya kutoa huduma kabambe, zenye usalama bila kuzingatia mipaka," alisema.

# Taasisi za fedha zatakiwa kutumia mifumo kidigitali

**Na Enock Charles**

BODI ya Michezo ya Kubahatisha nchini (GBT) imezitaka taasisi za kifedha kutumia mifumo ya kidijitali katika kufanya miamala ili kuendana na mazingira ya sasa na kuepuka uwezekano wa kueneza maambukizi ya magonjwa mbalimbali.

Miongoni mwa magonjwa hayo ni corona, ambao mpaka sasa bado ni tishio duniani.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na mwakilishi wa bodi hiyo, Elibariki Sengasenga, alipokuwa akiwapongeza washindi 12 wa Promosheni ya Benki ya NMB inayofahamika kama Masta Bata iliyofanyika, na kusema kwamba alisema Benki ya NMB imekuwa mfano wa kuigwa kutokana na kuhamasisha matumizi ya njia za kidigitali katika kufanya miamala ya kifedha, hivyo alizitaka taasisi zingine pia kufanya hivyo.

"NMB wamejaribu kutubadilisha kutuweka kidijitali, na kiukweli hakuna malalamiko yote, na ninawapongeza kwa hilo," alisema Sengasenga.

Kaimu Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki hiyo, Benedicto Baragomwa, alisema lengo la benki hiyo ni kuhakikisha usalama kwa wateja wao kuepukana na wizi na hata magonjwa hususan ambayo ni tishio hivi sasa.

"Dhumuni la promosheni hii ni kubadilisha tabia za wateja tunasema 'consumer behavior change' tunataka wateja kutotumia matumizi ya fedha taslimu kwa kuwa si salama sana kama ilivyo kutumia kadi, NMB tuna bidhaa tofauti zinazowezesha kulipa bila kutumia fedha taslimu kama NMB Mkononi na QR Code," alisema Baragomwa.

Katika kampeni hiyo washindi wa promosheni hiyo hupewa zawadi yenye thamani ya Sh. milioni 8 ambapo mshindi hujipatia televisheni ya inchi 50 iliyounganishwa na kifurushi cha bure, friji, kompyuta mpakato na simu aina ya Samsung A70 au kutembelea mbuga mojawapo ya wanyama kati ya Ngorongoro, Serengeti au kutalii Zanzibar.

# Wavamizi Bonde la Kilombero watimuliwa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI imewaagiza wananchi wote waliovamia katika Bonde la Ardhiovu la Kilombero lililopo wilayani Kilombero mkoani Morogoro na kufanya shughuli za kibindamu ikiwamo kilimo na ufugaji kuondoka mara moja vinginevyo watakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi.

Agizo hilo limetolewa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, wakati wa Siku ya Wanyamapori iliyoadhimishwa jana mkoani Morogoro na kushirikisha wadau wa utalii.

Waziri alisema eneo hilo lipo ndani ya hifadhi kwa ajili ya maliasili mbalimbali ikiwamo mimea, wanyama na baionuwai kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Dk. Ndumbaro alisema kutokana na umuhimu wa bonde kwa sasa ndio tegemeo kubwa kwa asilimia 65 ya maji yake na mito inategewa kutitirisha katika bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere, aliwataka waliovamia na kufanya shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo na ufugaji kuondoka mara moja.

"Hilo bonde la Kilombero limetengwa tangu miaka ya nyuma kwa ajili ya ardhioevu, zipo maliasili nyingi, ikiwamo mimea isiyopitikana duniani, baionuwai mbalimbali na wanyama kama sheshe, lakini watu wamevamia na kufanya kilimo na ufugaji... sasa tunawaambia waondoke haraka sana, vinginevyo watakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi," alisema Waziri Dk. Ndumbaro.

Alisema licha ya mafanikio hayo, lakini bado changamoto kubwa ni kuvamiwa kwa maeneo ya hifadhi yaliyotengwa, na kwamba mfumo wa ardhi nchini ni mali ya Rais, hivyo taasisi zimetengewa ardhi hizo kwa mujibu wa sheria na wananchi hawapaswi kuanzisha migogoro kwa ajili ya kuhalalisha upataji ardhi.

Akizungumzia kuhusu sekta ya utalii, alisema kwa sasa imepata mafanikio makubwa na kuchangia katika pato la Taifa kutokana na kusaidia kukomesha ujangili kwa asilimia 90 na mikakati ya kufikia asilimia 100 tayari imewekwa.

Naye Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA, Dk. Allan Kijazi, alisema siri kubwa ni uwekezaji mkubwa kwenye uhifadhi, uboreshaji na utoaji wa huduma bora kwa watalii ambao unajikita kuwezesha watalii kufurahia wanapofika maeneo ya utalii nchini.

Kwa upande wake Kamishna Mhifadhi wa Misitu kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TSF), Prof. Dos Santos Silayo, alisema kuwa wataendelea kuongeza ulinzi katika misitu kutokana na umuhimu wake hasa katika kulinda ikolojia mbalimbali za wanyamapori kwa kuwa vinategemeana.




Meneja Mauzo Mafuta ya Ndege wa Kampuni ya Puma Energy Tanzania, Rehema Migambile (wa pili kushoto) na wafanyakazi wenzake, wakiwa wameshika cheti cha mafunzo ya wanawake katika uongozi, baada ya kutunukiwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani), katika mkutano mkuu wa tatu wa wanawake katika uongozi, uliondaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), jijini Dar es Salaam jana, ambapo wanawake 64 kutoka kampuni na mashirika mbalimbali walishiriki mafunzo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TADB, WFP wajadili uwezeshaji wanawake, vijana kwenye kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula (WFP), jana waliendeleza mashauriano yao juu ya mbinu za kuwawezesha wanawake na vijana ili wanufaike na mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo.

Mashauriano hayo yalifanyika jijini Dar es Salaam sambamba na shughuli za juma zima za kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani zinazofikia kilele chake Jumatatu.

Mazungumzo hayo yaliwakutanisha Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine na Mwakilishi Mkazi wa WFP nchini, Sarah Gordon-Gibson, ambaye aliambatana na Mkuu wa Usimamizi wa Ugavi wa WFP, Riaz Lodhi.

"Nina furaha kubwa kurudi Tanzania. Nchi hii ilibarikiwa na rasilimali nyingi na yenye uwezo wa kufanya mambo makubwa. Ninatarajia kufanya kazi na TADB kwa ukaribu sana, hasa hasa kwenye suala la ongezeko la thamani la mazao ya kilimo nchini, ili tuweze kuona namna ambavyo wakulima, hususan wanawake na vijana wanavyoweza kunufaika, maana wao ni kiungo muhimu katika kupunguza umaskini na uletwaji wa maendeleo nchini," alisema Gibson.

Kwa upande wake, BJustine alikaribisha ushirikiano mpya na taasisi hiyo ya chakula iliyo chini ya Umoja wa Mataifa, na alisisitiza utoaji wa msaada wa kiufundi na kiutaalamu kutoka WFP ili kuongeza ufanisi na unufaikaji kwa wakulima kupitia miradi mipya na inayoendelea kutekelezwa na benki hiyo.

"Tunahitaji kujenga mifumo ili kufanya kilimo kiwe endelevu. Hii ni sababu kubwa ya sisi kushirikiana na wadau wa maendeleo kama WFP ili kufikia malengo hayo. Tunahitaji kuwekeza kwa ajili ya vizazi vijavyo si tu vya sasa," alisisitiza Justine.

Taarifa iliyotolewa na TADB imesema mashauriano ya jana yalihusisha namna ya kuwawezesha wanawake na vijana ili wanufaike na mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo. Kadhalika, wajumbe walizungumzia uongezaji wa msaada wa kiufundi na kiutaalamu wa WFP katika miradi inayogharamiwa na TADB, na pia walijadili uwezeshaji unaolenga ongezeko la thamani la mazao ya kilimo nchini Tanzania katika ujumla wake.

HABARI KITAIFA

# Wazoa fedha NMB Bonge la Mpango

**Na Mwandishi Wetu**

DROO ya kwanza ya Kampeni ya Weka Akiba na Ushinde inayoendeshwa na Benki ya NMB iitwayo Bonge la Mpango, imefanyika leo, ambako washindi 10 wameshinda fedha taslimu na wawili wakijitwalia pikipiki ya tairi tatu aina ya Lifan Cargo.

NMB Bonge la Mpango, inalenga kutambua na kuthamini utamaduni chanya wa wateja kujiwekea akiba, ikiwa ni pamoja na kurejesha sehemu ya faida ya benki hiyo kwa mwaka uliopita, ambako NMB ilipata faida ya zaidi ya Sh. bilioni 205.

Akizungumza wakati wa droo hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Ally Ngingite, aliwataka wateja wa benki hiyo kuendelea kujiwekea akiba mara kwa mara, ili kujishindia zawadi mbalimbali zenye thamani ya Sh. milioni 550.

Ngingite alibanisha kuwa ukiondoa fedha taslimu wanazoshinda wateja wa kila wiki, NMB Bonge la Mpango pia inawawezesha wateja wawili wa kila wiki kushinda pikipiki ya mizigo, gari dogo la mizigo aina ya Tata 'kirikuu' na Toyota Fortuner.

"Wito wetu kwao ni kudumsha utamaduni wa kujiwekea akiba, ili kujishindia pesa taslimu, pikipiki aina ya Lifan Cargo, kirikuu na Toyota Fortuner.

"Ukiweka kuanzia Sh. 100,000 unakuwa na nafasi ya kushinda fedha taslimu, pikipiki ama kirikuu na wale ambao akaunti zao zitakuwa na akiba isiyopungua Sh. milioni 10, watashindania Toyota Fortuner ya Sh. milioni 169," alisema Ngingite.

, Ofisa kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Elibariki Sengasenga, aliipongeza NMB kwa kampeni zilizobeba uwezeshaji kwa wateja, huku akiwahakikishia washiriki kuwa droo hizo zinafuata taratibu zote.

"Tunawahakikishia wateja wa NMB kuwa droo hizi zinasimamiwa na GBT kwa kufuata taratibu na hakuna ubabaishaji wowote. washindi watapatikana kutokana na bahati zao tu na si vinginevyo."

# Mabomba ya maji ya ubora yatakiwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

NAIBU Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, amewataka wamiliki wa viwanda vya ndani vya utengenezaji wa mabomba ya maji kuhakikisha wanazingatia ubora na viwango vinavyohitajika ili kukidhi soko la ndani na kuleta tija katika ujenzi wa miradi ya maji.

Mahunda, aliyabainisha hayo alipotembelea na kukagua shughuli za uzalishaji wa mabomba ya maji katika kiwanda cha utengenezaji wa bidhaa hizo kinachomilikiwa na Kampuni ya Kahama Oil Mills (KOM) Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga.

Aidha alisema, Wizara inaendelea kutumia mabomba yanayozalishwa na viwanda vya ndani katika utekelezaji wa miradi ya maji inayoendelea kujengwa nchini, na kwamba kutokuzingatia viwango vya utengenezaji wa mabomba hayo yanatumika kwa muda mfupi na kupasuka.

"Moja ya viwanda tunavyotumia bidhaa wanazotengeneza katika kutekeleza miradi yetu ya maji na hiki nimojawapo...sisi wizara tunaomba mzalishe mabomba imara ambayo hayatapasuka tutakapoyatumia, lengo ni kuwaunga mkono wawekezaji wazawa kwenye shughuli wanazozizalisha," alisema Mahundi.

# Wakulima wa kahawa wapinga kulipiwa benki

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

BAADHI ya wakulima wa kahawa katika Kata ya Kishanje Bukoba Vijijini, wameiomba serikali kubadilisha mfumo wa kulipwa fedha kupitia benki, wakidai unawasababishia usumbufu kutokana na maeneo ya vijijini kutokuwa na huduma za kibenki.

Wakitoa kero zao kwa Mbunge wa Bukoba Vijijini, Jasson Rweikiza, wakulima hao, walisema kuwa wanapouza kahawa yao kupitia vyama vya ushirika vya msingi wanalipwa kupitia benki, hali inayowafanya kulazimika kusafiri kwenda mjini kutoa fedha katika akaunti, wakati wengine ni wazee.

"Zamani tulikusanya kahawa yetu na kulipwa tukiwa pale pale kwenye vyama vya ushirika vya msingi, lakini sasa tunakusanywa na kuambiwa tunalipwa kupitia benki, hapa tunapoishi benki hakuna inabidi kwenda mjini Bukoba, wakati wengine tumekwishazeeka, huu ni usumbufu kwetu," alisema Ferdinand Banobi.

Akizungumzia changamoto Rweikiza aliahidi kukaa na kuzungumza na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, ili kupata njia nyingine mwafaka ya kutoa malipo hayo, bila kuwaumiza wakulima hasa wazee.

"Lakini wahusika nao wanajitetea kwamba kubeba fedha kwenye mafurushi kwenda kuwalipa wakulima sio salama ni hatari, kwa hiyo itatafutwa njia nzuri mbadala inayokubalika ili kuwasaidia wakulima wasipate taabu," alisema Rweikiza.

Alisema mkulima kwenda mjini ni mbali, na kwamba kuna kipindi walianza kuwalipa kwa simu, lakini pia utaratibu huo haukufaa kutokana na baadhi ya mawakala wa vijiji walipo wakulima, kutokuwa na fedha za kutosha.

"Mfano Izimbya nikiwa kule kuhudumia wananchi wangu, kuna mzee mmoja alilipwa pesa za kahawa kwa simu zaidi ya Sh. 800,000, alikwenda vibanda vyote vya pale, lakini hakufanikiwa kupata, akalazimika kurudi nyumbani bila pesa wakati anazo kwenye simu," alisema.




Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Ally Ngingite (katikati), akizungumza wakati wa kuchezesha droo ya kwanza ya Weka Ushinde Bonge la Mpango inayoendeshwa na benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkaguzi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Elibariki Sengasenga na Ofisa Huduma kwa wateja wa benki hiyo, Neema Deusi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aja juu mil. 356/- za wakulima wa korosho

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani Mhandisi Evarist Ndikilo, amemtaka mmiliki wa Kampuni ya Mafubilo General Supplies iliyopo Kibaha kuwalipa wakulima wa korosho Sh. 356,156,335.30

Fedha hizo ni deni wanalodai wakulima wa Kibaha baada ya korosho zao kilo 282,306.5 zilizokuwa kwenye vyama vya ushirika (Amcos) vitano kuuzwa kwa kampuni hiyo.

Ndikilo alitoa agizo hilo Mjini Kibaha wakati wa kikao maalum na wakulima ambao waliingiia mkataba na muwekezaji huyo.

Kutokana na deni hilo Ndikilo alitoa wiki moja kwa muwekezaji huyo kukiri kuwa atalipa deni hilo atakapopata barua ya kumtaka alipe.

Aidha, amempa miezi mitatu kuhakikisha analipa deni hilo, na akishindwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Alimtaka mmiliki wa kampuni hiyo kulipa fedha hizo kwa awamu tatu kila awamu ahakikishe analipa Sh. milioni 118. Kwa mujibu wa mkataba uliosainiwa Februari mwaka 2020 kati ya Kampuni ya Mafubilo na vyama hivyo, mnunuzi alitakiwa kulipa fedha hizo kwa siku 63.

Amcos zilizoshiriki kusaini mkataba huo ni Kongowe (kilo 168,982.50), Mwendapole (kilo 2,279), Misugusugu (kilo 72,314), Visiga (kilo 36,244) na Mkombozi (kilo 2,487) na kwamba kilo zote zina thamani ya Sh. 394,156,335.30. Hadi sasa ni Sh. milioni 40 tu ambazo zimelipwa na Kampuni hiyo.

# SIDO Mtwara yawawezesha vijana kaya maskini

**Na Ziwena Shame**

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) Mkoa wa Mtwara, limewawezesha vijana 14 kutoka kaya maskini na mazingira magumu kupata mafunzo ya ujasiriamali.

Mafunzo hayo yenye lengo la kuwainua kiuchumi vijana kutoka kaya maskini ambazo zinanufaika na mpango wa kunusuru kaya masikini unaosimamiwa na mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) sehemu ya pili awamu ya tatu.

Akifunga mafunzo hayo yaliyofadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa (TEA), Kaimu Meneja wa Shirika hilo, Twaha Sued, alisema mafunzo hayo ya mwezi mmoja yalijumuisha vijana kutoka Wilaya ya Mtwara.

Alisema serikali kupitia TEA iliona umuhimu wa vijana hao kupata mafunzo kwa sababu wanatoka katika kaya maskini na pia itachangia kuinua kipato cha familia, hivyo kuwapatia vifaa vya kuanzia kazi.

Alisema vijana hao wamejifunza kutengeneza batiki, siagi ya karanga na korosho, achali ya embe, sosi ya nyanya, sosi ya pilipili, unga wa lishe na keki na batiki za aina mbalimbali.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Wilaya ya Mtwara, Thomas Salala, amewataka vijana hao kuitumia nafasi hiyo kufanyakazi kwa bidii ili kubadilisha maisha yao na familia zao kwa kuunda vikundi ili kufanyakazi kwa kushirikiana.

# Wanahabari wapewa mbinu uandishi habari za wanawake

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAANDISHI wa habari Pemba wametakiwa kujua sera, katiba, sheria na vifungu vyake ili kuwasaidia kuzitumia katika kuandika habari zao za wanawake kushiriki katika uongozi.

Akiwasilisha mada katika mafunzo ya waandishi wa habari juu ya kuwajengea uwezo wanawake kudai haki zao za kisiasa na uongozi, Mwanasheria Mohamed Hassan Ali alisema, kujua vifungu vya sera, sheria na katiba ni muhimu sana kwa waandishi.

Alisema Serikali zote mbili ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano zimempa fursa mbalimbali mwanamke, ikiwamo kuwa kiongozi, hivyo ni muhimu kwa waandishi kutumia vifungu hivyo wanapoandika habari zao, ili jamii ielewe kwamba wanawake nao wana haki ya kuwa viongozi.

"Kwa kweli ni wenyewe tu wanawake hawajaamua au tuseme walikuwa hawajui, lakini sera, katiba na sheria za nchi zimetoa fursa kwa mwanamke, hivyo tuchukue juhudi kuhakikisha wanawake wanaingia katika uongozi," alisema.

Aidha, alisema kuna mikakati mbalimbali ya uteketezaji wa haki, sera na maendeleo ya wanawake na jinsia katika siasa, uongozi, utawala na kujitetea, hivyo hakuna sababu ya wanawake wasishiriki katika masuala ya uongozi.

Akiwasilisha mada ya demokrasia, mwanaharakati Sabah Mussa Said, alisema mwanamke ndie mhusika zaidi katika ustawi wa jamii, hivyo inahitajika kumuandaa mtoto wa kike mapema, ili kuwajenga vizuri katika kupata viongozi bora. "Tuliwaacha kuwaandaa watoto wetu mapema na ndio maana tukawanyima kidogo kwenye vyombo vya kutoa uamuzi, waandishi tuielimishe jamii, tusiangalie juu juu tu, kwani bado tuna safari ndefu ya kuhamasisha", alisema.

Nae akiwasilisha mada ya takwimu Katibu wa Klabu ya Waandishi wa habari Pemba (PPC), Ali Mbarouk Omar, alieleza kuwa, ukosefu wa mtaji na rasilimali unawakwaza wanawake kuingia katika uongozi, hivyo wanahitaji kujengwa na kuwezeshwa kwa kila nyanja kufikia malengo.

"Tunapoandika habari zetu tuzingatie takwimu, hii itatusaidia kuandika kwa usahihi, kueleza watu ukubwa wa jambo na pia unasaidia watu kujielewa", alifahamisha.

Mapema akifungua mafunzo hayo Mratibu wa Chama Cha Waandishi wa habari Wanawake Tanzania (TAMWA) kwa upande wa Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema mradi huo ni wa miaka minne wenye lengo la kuongeza uhamasishwaji wa wanawake katika demokrasia na uongozi, ambapo wanatarajia kuwafikia watu 6,000.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Japhet Justine (kulia), akizungumza na Mwakilishi Mkazi mpya wa Shirika la Chakula Duniani (WFP) nchini, Sarah Gordon-Gibson (katikati) na Mkuu wa Usimamizi wa Ugavi wa WFP, Riaz Lodhi, ujumbe huo ulipotembelea benki hiyo jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TASAF yamnusuru kukosa masomo ya chuo kikuu

**Na Marco Maduhu, SIMIYU**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umemsaidia Barnaba Salamba, mkazi wa Mtaa wa Kiwanja cha Ndege wilayani Maswa mkoani Simiyu, kumaliza masomo yake katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA).

Ofisa Ufuatiliaji wa TASAF katika Halmashauri ya Maswa, John Wambura, alisema juzi kuwa halmashauri hiyo imesaidia vijana 10 kusoma masomo yao ya chuo kikuu, akiwamo Salamba ambaye alikuwa amekata tamaa na kurudi nyumbani.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa kutoka kwa mtumishi mwenzao wa halmashauri kuwa kuna kijana ambaye wazazi wake ni walengwa wa TASAF ameshindwa kuendelea na masomo ya chuo kikuu kutokana na kukosa ada na kuamua kurudi nyumbani, walimfuata na kumsaidia kurudi chuo.

"Fedha ya ruzuku ya TASAF huwa ina masharti ya ukomo wa utoaji elimu kwa watoto wa walengwa wetu, ambapo husaidiwa kuanzia elimu ya msingi hadi kidato cha sita tu.

"Lakini kwa hawa wanafunzi ambao wapo ngazi ya chuo kikuu, sisi huwa hatutoi fedha, bali tunawaandikia barua na kuipeleka kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili wapate mkopo haraka na kwa asilimia 100," alisema.

Wambura alisema walimsaidia Salamba kupata mkopo kwa asilimia 100 na hatimaye kufanikiwa kurudi chuoni kuendelea na masomo yake na mwaka jana alihitimu.

Salamba, akisimulia ugumu wa maisha ambao aliupata chuoni, alisema kuwa kabla ya kuamua kurejea nyumbani, alikuwa akisoma bila usajili kwa kuwa hakupata pesa ya kulipa ada, huku akipata chakula kwa shida.

Alisema kuwa baada ya kuwasiliana na wazazi wake na kumweleza kwamba wamekwama, ndipo akaona hakuna haja ya kuendelea na masomo na kuamua kurudi nyumbani kujikita kwenye kilimo.

Alisema baada ya kusaidiwa na TASAF na kupata mkopo wa masomo kwa asilimia 100 ndani ya miaka mitatu akisomea taaluma ya misitu, alirejea chuoni na sasa amehitimu na ana mikakati ya kujiajiri mwenyewe kwa kuanzisha kiwanda cha mbao.




Ukurasa 12

Msitu utalii uliosheheni utajiri uchumi, lakini wengi hawaujui



Ukurasa 13

Kulikoni hoja kudai azidishe muda?

BUFE

IJUMAA MACHI 5, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

Mteja mfalme biashara ya simu za mkononi

KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE

# Walionasa waibuliwa na mdau hadi kufikia makuu ya kuigwa

**Na Yasmine Protace**

TAASISI zinazowasaidia vijana elimu ya ujasiriamali, zimekuwa zikiwaokoa wengi kujiajiri wakihama kutoka vijiweni. Hapo kuna mafunzo na kuwanoa wakizaliwa upya na mengineyo mengi.

Kanuni ya kimaisha, mara zote inatakiwa kila anayepata fursa kuwa mahiri wa kuitumia katika msamiati wa 'kujiongeza' kwani ishara ya ukombozi wao kiujumla.

### UNDANI WA SIMULIZI

Hawa Sindika miaka (28), mkazi wa Tegeta Dar es Salaam, anayejitambulisha kuwa na elimu ya juu bila ya kuifanua. Hata hivyo, suala la kuajiriwa lilibaki mtihani kwake, ingawa hakukata tamaa.

Anasema ndani ya elimu yake hiyo, aliamua kufanya biashara ya kuuza nazi kwa kuzitoa katika mikoa ya kusini mwa nchi na kuwauzia wafanyabiashara wa kawaida.

Hapo ndipo alipoona tangazo kutoka Asasi ya Restless Development jijini Dar es Salaam, lililowataka vijana wa kujitolea. Naye akaomba fursa.

Anaendelea: "Nilipoipata nafasi hiyo, nilipatiwa mafunzo ya kujiajiri na kuajirika, ndipo nilipoweza kuaminiwa na mashirika mengine, kufanya nao kazi. Nikafanikiwa kupata mafunzo mengi zaidi ya biashara na kuanzisha biashara," anaeleza.

Hawa anasema, hatua iliyofuata, alianzisha kiwanda kidogo cha kutengeneza mafuta ya nazi, kilichopo Sinza kwa Remmy, jijini Dar es Salaam. Hapo anatamba kwa usemi "mwanamke akiwezeshwa anaweza" akisema anakuwa wa mfano, kwa kinamama.

Katika kiwanda hicho kinachozalisha lita 100 za mafuta, kila baada ya siku nne, kimeajiri vijana sita wa kudumu na vibarua watano.

Anasema katika kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, inayoadhimishwa kila Machi 8 ya mwaka (Jumatatu ijayo), anawataka kinamama kufuatilia fursa wanazotangaziwa, ili ziwanufaishe.

Kwa sasa, Hawa anaweka shukurani ya kwanza kwa Asasi ya Restless Development, iliyomfanikisha, hivi sasa akiwa ni kioo cha mafanikio kwa kumiliki nyumba ya makazi na anatoa rai ya wapanue fursa hizo kwa vijana zaidi.

Ni biashara zake anayoifanya ndani na nje ya nchi, ikiwamo Sweden, huku wateja wengine akiwa nao katika hatua ya maongezi ya soko.

Anataja changamoto kuu kwake ni baadhi ya taasisi za mikopo kuwa na masharti magumu. Mwingine ni Dorice Mkiva, mkazi wa Temeke, Dar es Salaam anajitaja kuwa mwezeshaji mradi wa 'Kijana Wajibika' kupitia Asasi ya Restless Development.

Anasema malengo ya mradi ni kuhakikisha kunakuwapo ujumuishi katika nyanja za uongozi na kuhakikisha vijana wanapata fursa ya kushiriki miradi na unafanyiwa kazi na taasisi za kijamii, ili kuhakikisha inafikiwa kwa mapana zaidi.



Kinamama wakiwa katika shughuli za ujasiriamali. **PICHA: MTANDAO**

Mama huyo anataja wajibu wake ni kushawishi ofisi zao taasisi za kijamii kuwa na usawa kijinsia kwenye uongozi ofisini na miradi, pia kuwashirikisha walemavu.

Anasema, Restless Development inazingatia ujumuishi kwa wenye ulemavu, ikiwamo kuwasaidia kushiriki kwenye mikutano inayolenga fursa na uongozi.

Dorice anatumia maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, akidai itumike kuwasogeza mbele, sambamba na wadau wao wenye ulemavu.

Hivi sasa mama huyo anajivunia manufaa kama ya mwenziwe Hawa, kwamba Restless Development imempatia ujasiri. Sasa anageuza uso wa kukosoa baadhi ya asasi zinazokwepa kuwasaidia wenye ulemavu.

Anataja ndoto yake ni kuwa mfanyabiashara wa chakula na sasa anaomba msaada wa baiskeli ya magurudumu matatu kumwezesha kuwajibika.

Dorice anawataja wabia wake kazini sasa ni mabinti walioacha masomo kutokana na ujauzito, hivyo wana hali ngumu kimaisha.

Anafafanua kuwa asasi aliyo nayo kikazi ina mpango maalum wa kuwasaidia mabinti waliopata ujauzito na wakatelekezwa, wamesaidiwa na kufanikiwa.

"Pia, tumeona mabinti wanarubuniwa na tumekuwa tukiwapatia elimu ya jinsia, ili wajikinge na magonjwa," anasema Dorice, huku akitaja maeneo yao hatari ni maambukizi kama ya maradhi UKIMWI. Wanawasaidia kwa kuwafikia na kuwahudumia mahali waliko.

Ramlati Omary, mkazi wa Mbagala, Dar es Salaam, anasema alianza kufanya kazi na RD tangu mwaka 2016, hadi mwanzoni mwak 2020, akidumu kama Mwelimisha Rika.

Anasema, ni mradi uliopatia elimu tofauti, ikiwamo katika sekta za elimu, afya, uongozi, ujasiriamali, utambuzi wa stadi za maisha.

Hivi sasa anasema, anatumia ujuzi huo katika jukumu la ajira binafsi, akitengeneza batiki na sabuni za maji, soko lake kuu ni maofisini, kwenye baa, majumbani na nyumba za kulala wageni, sambamba na kutoa mafunzo ya utengenezaji sabuni na batiki katika makundi ya vikoba.

Naye katika eneo hilo, anataja changamoto yake kuu ni kasi kuu ya ushindani wa kuuza bidhaa sokoni.

UCHUMI

VIKINDU

# Msitu utalii uliosheheni utajiri uchumi, lakini wengi hawaujui

## • Umri miaka 78, umbali 'jicho na pua' • Wako nyoka tishio, mbega, vipepeo, miti...

**Na Beatrice Philemon**

UNAPOZUNGUMZIWA Msitu wa Hifadhi Vikindu, huenda siyo wananchi wote wa wilaya Mkuranga mahali na majirani wa jiji la Dar es Salaam.

Ni eneo kulikotengwa kwa ajili ya hifadhi ya misitu na viumbe vinavyopatikana humo, ili visiharibiwe na shughuli za binadamu, pamoja na rasilimali za misitu zinazopatikana.

Msitu huo wa Mkuranga ulioko katika kata ya Mwandege, Pwani, uko umbali wa kilomita 17 kutoka mpakani mwake na Dar es Salaam. Ni kati ya misitu minne iliyopo wilayani Mkuranga, inayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Mhifadhi wa TFS Mkuranga, Charles Kaselya, anaiambia Nipashe kwamba ulianzishwa mwaka 1947 na serikali ya kikoloni wakati huo, ukiwa na ukubwa wa hekta 1,690. Wakati huo ulitwa Msitu wa Lindi Maji (Catchment).

Kiojiografia, unapakana na vijiji vitano: Vikindu, anavyovitaja kuwa ni: Mwandege, Mlamleni na Luzandu.




Picha tofauti za ziara na utalii, ndani ya Msitu wa Hifadhi Vikindu, ulioko Mkuranga mkoani Pwani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### NAMNA ULIVYO

Kaselya anasema, hivi sasa TFS imeshaanza kutangaza utalii wa ikolojia katika Msitu wa Hifadhi Vikindu, kuvutia watalii wa ndani na nje watembelea eneo hilo.

"Vivutio vya utalii vinavyopatikana katika msitu huu ni wanyama na wadudu wa aina mbalimbali wakiwamo kima, tumbili, digidigi, nguruwe pori, ngiri, paa, nguchiro, nyoka aina ya chatu, black mamba, mbega weusi na weupe, ndege wa aina mbalimbali, vinyonga na vipepeo.

Pia, kuna aina 65 za miti ya asili tofauti kwa ajili ya dawa za asili na mbao, huku kukiwapo mabwawa makubwa ya asili mawili yenye samaki kama perege, kambale, pweza, vibua na vyura.

Mengine katika hilo yanatajwa kujumuisha mito isiyokauka mwaka mzima, daraja la asili lenye urefu ita 52 katika Mto Mkangazi na mbuyu wa matambiko.

Orodha ya miti asili inayopatikana mahali hapo inajumuisha mkongo, mkunachuma, mtete, mpilipili, Mkuruti, Mkwee/Uswee, Mtalala, Mbula na Mtunda.

> **"Mbuyu huu zamani ulikuwa ukitumiwa sana na wazee wakati wa ukame kuomba mvua kipindi cha ukame.**

Katika hiyo, Kaselya anasema kuna baadhi ya miti katika msitu huo ni bora kwa ajili ya dawa za asili na upasuaji mbao na hairuhusiwi kuvunwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya utalii au ikolojia na utafiti.

### VIVUTIO VYAKE

Anawaomba wakazi wa Dar es Salaam kupatembelea washuhudie vivutio vingi, ikiwamo kambi za watalii. Kwa sasa kambi za watalii za Hifadhi za Vikindu zipo mbili; Mkangazi na Mbuyu.

"Kambi ya Mkangazi imeendelezwa kwa kujengwa choo, kisima kibanda cha mlinzi, viti vya watalii na kupandwa nyasi za asili na maua.

"Uendelezaji zaidi unaendelea kufanyika ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kutajengwa msonge mmoja, jiko, ukumbi wa kulia chakula na ofisi ya mapokezi," anasema.



Pia, kunaelezwa kambi ya Mbuyu bado haijaendelezwa kutokana na ufinyu wa bajeti na TFS inatarajia kujenga minara mitatu ya utalii msituni Mwandege, Churwi na Jibrota, ili kuwawezesha watalii kupanda na kuona mandhari ya msitu wote na Dar es Salaam

"Mnara utakaojengwa churwi utamwezesha mtalii kuona manzari ya jiji la Dar es Salaam ikiwapo Bandari," anasema Kaselya.

Pia, anasema TFS ina mpango wa kutengeneza bustani ya vipepeo msituni ili kuwavutia watalii wengi kutoka Bulgaria na kwingineko wanaozuru kuangalia vipepeo, pia kupiga picha.

Anaelezea kuwapo madaraja ya kutegenezwa na mbao yenye upana wa mita 52, zilizopita kwenye Mto Mkangazi pia Mto Binguni, vyote kwa pamoja vyanzo vyake ni chemchemi kutoka Msitu wa Vikindu,

Kaselya anasema, mito hiyo ya maji haikauki kipindi chote cha mwaka, huku Mkangazi ukiwa kivutio cha utalii wa ndani na nje, ambako kunapatikana mbuyu wa matambiko ya asili tangu zama zilizopita na zitumiwa na wenyeji kutambika na kufanya maombi matatizo na tiba mbalimbali za kiasili.

"Mbuyu huu zamani ulikuwa ukitumiwa sana na wazee wakati wa ukame kuomba mvua kipindi cha ukame," anasema.

### TFS YAJIPANGA

Ofisi ya TFS Mkuranga inaendelea kuweka mipango ya kutangaza vivutio kwenye bonanza na mikutano ya kijamii na inayoishi karibu na msitu, kuipatia elimu na kuihamasishia utalii wa ndani na matukio hasa katika sikukuu za kitaifa.

Hiyo inalengwa kufanyika katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, jambo linaloaminika litaongeza upatikanaji wa wageni wanaotembelea Hifadhi ya Msitu Vikindu.

### UTALII MSITUNI

Ofisa Utalii, Msitu wa Hifadhi wa Vikindu, Kassim Litonya, anasema serikali imeshafungua utalii kwenye msitu wenye vivutio vingi na viingilio nafuu.

Mchakato wa kuanzisha utalii Ikolojia katika msitu wa hifadhi wa Vikindu ulianza mwaka 2015, kwa kusafisha njia za kutembea watalii zenye urefu wa kilomita 15 kwenda kwenye maeneo ya vivutio, kujenga madaraja na maeneo ya kambi za watalii.

Watalii wamekuwa wakiongezeka hasa kuanzia Mwaka 2019/2020 ndiyo kumekuwa na watalii wa ndani na nje wanaotembelea Hifadhi ya Msitu huu.

"Hadi sasa TFS imefanikiwa kujenga mabanda ya kupokea watalii na kufungua vivutio vya utalii ikiwamo mabwawa ya asili 'camp sites', vituo vya kufundishia uhifadhi wa miti ndani ya msitu, kwenye vitalu na kuonyesha aina ya miti, anasema

Watalii wana fursa ya kutembelea msituni, mito na mabwawa yasiyokauka humo kwa kipindi cha mwaka mzima, vivyo hivyo, katika kambi mbili zilizomo humo anazozitaja kuwa Mbuyuni na Mkangazi.

Mkurugenzi wa taasisi isiyo ya kiserikali- Pwani Medication Awareness Organization (PWAMAO), Salum Kitika, aliyeambatana na watalii wa ndani 18 kutoka mashirika mbalimbali, anasema waliamua kutembelea msitu huo kushuhudia vivutio vya msituni na kuhamasisha jamii itembelee.

Kitika anawataka watu wajifunze mambo mbalimbali yanayohusu mimea na kutangaza vivutio vilivyopo, hali inayotoa hamasa na wrngine nao kutaka kupatembelea.

"Wakati wa ziara nimeona vitu ambavyo sijawahi kufikiria kama vitakuwepo ndani ya eneo hili, ingawa naishi kilomita tano kutoka kwenye msitu," anasema

Anataja vingine vya kuvutia ni mabwawa mawili ya asili, mimea, ndege, wanyama, chatu, madaraja ya asili na mjumuiko wa watu mbalimbali, watokao sehemu tofauti.

"Kitu ambacho kilinivutia katika ziara hii ni nyimbo kutoka kwa waongozaji wa bwawa la asili la Miwaleni, ambako kuna samaki wa asili," anaongeza Kitika.

TFS inasema imezindua utalii wa ikolojia msituni humo, kwa sababu watu wengi ndani na nje ya Mkuranga, hawakujua uwapo wa kivutio hicho.

Huku akisifu ni mazingira yanayofaa pia kwa michezo ya riadha ndefu, maarufu 'marathon', pia anaongeza kunafaa kwa mazoezi ya mbio (jogging).

"Hivi karibuni tutaandaa forest marathon (mbio ndefu za poroni) ambayo tutaitangaza hivi karibuni. Lengo ni kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo ndani ya msitu huu jirani na jiji la Dar es salaam, kwani ni sehemu unayoweza kufika kwa urahisi na mabasi," anahitimisha.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Kulikoni hoja kudai azidishe muda?



MITANDAO ya kijamii imekuwa njia rahisi sana kwa jamii kuwasiliana kuhusu masuala mbalimbali yanayotokea kinadharia na kivitendo, yakiwamo yanayoelimisha, kuburudisha na kutaarifu, ili mradi yote yana nia njema kwa jamii husika.



NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

Taarifa zinazotolewa katika mitandao hiyo, zinaanzia katika majukwaa mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na hata kijamii, yakiwamo ya kitaaluma na huzaa majadiliano yanayoishia kukubaliana au kutokubaliana.

Mijadala mingine husababisha ukakasi wa hali ya hewa kisiasa na hata kijamii na kufikia hatua ya baadhi ya waanzilishi wa hoja hizo kuchukuliwa hatua za kisheria, kutokana na kutozingatia maadili au taratibu zilizoteuliwa kufuatwa katika muktadha husika.

Kuna mijadala imekuwa ikibeba uzito sana katika mitandao hii, kwani inaonekana kuwa rahisi kujadilika na kuzua ubishani, unaozaa pande mbili hasi na chanya na hata kuishia kutokubaliana, ingawa inwezekana pia kusaidia kufumbua macho na hata kuelimishana.

Katika Bunge la 12 kwenye mkutano wake wa kwanza ulioanza Februari 2, 2021, Mbunge wa Makambako, Deo Sanga (CCM) akichangia hotuba ya Rais ya Ufunguzi wa Bunge hilo, alitamka mema na mazuri aliyofanya Rais John Magufuli katika kipindi chake cha uongozi na kutaka aongezwe muda wa urais, hata atakapokuwa utakapogota kwa mujibu wa Katiba.

Sanga akatumia msamiati wake linganishi bengeni, katika mtazamo kama ilivyofanyika China ambako Rais wa nchi hiyo sasa ni wa maisha.

Hata hivyo, akiongoza kikao cha siku hiyo, Naibu Spika Tulia Ackson, aliwakumbusha wabunge kukumbuka msimamo wa Rais Magufuli.

Naibu Spika alisema kauli ya Sanga ni yake binafsi, lakini ni vema kuheshimu msimamo wa Rais. Dk. Magufuli alishasema si mara moja au mbili, kwamba hataongeza hata dakika moja, tena akisisitiza kuwa kazi ya urais ni ngumu na hivyo kipindi chake kitakapokoma, ataondoka bila ya kuchelewa.

Kauli ya Sanga ilishapata kutolewa, pia na wabunge wa zamani, Juma Nkamia, Ally Keissy na Kangi Lugola. Lakini, kila mara zilipokuwa zikitolewa, kwenye mitandao ya kijamii, iliwekwa kauli ya Mwalimu Julius Nyerere ikisema:

"Kila nilipokuwa nataka kung'atuka walikuwa wakiniambia: 'Mwalimu endelea tu, hii nchi ni changa na umeitoa mbali. Nchi hii haitaendelea bila wewe.' Niliendelea hadi pale nilipokuja kugundua kumbe nchi changa waliyoiongelea ni familia zao na hazitaendelea bila mimi kuwapo madarakani, maana walikuwa hawana uhakika kama Rais ajaye atawaacha katika nafasi walizokuwa nazo."

Kauli hiyo ya Mwalimu Nyerere, inaonekana kuwa bado na mashiko, nadhani hata Rais Dk. Magufuli, anakumbwa na hisia kama hiyo na ndiyo sababu kila mara amekuwa akikataa wazo la kuongezwa muda.

Naamini, Dk. Magufuli anajua nini maana ya demokrasia na nini Katiba inataka, huku akitambua kuwa nchi hiii na Watanzania karibu milioni 60 na haitawezekana kukosekana mtu atakayeendeleza mema atakayoyaacha, kama anavyofanya yeye.

Naamini naye atahitaji kupumzika, ili abaki kutoa ushauri kama waastaafu waliomtangulia wanavyofanya. Alamsiki!

UCHUMI

# Mteja mfalme biashara simu mkononi

Na Mary Geofrey

- Watoa huduma wabanwa kwenye ukweli
- Utapeli kwenye simu pingu yao rasmi jirani
- Aprili Mosi mambo 12 kuanza kutekelezwa

MAMLAKA ya Mawasiliano (TCRA), mdhibiti wa sekta ya mawasiliano ya kielektroniki na posta nchini, hadi sasa ndio msimamizi muu wa tozo na ufanisi wa huduma za mawasiliano nchini.

Hivi karibuni kumekuwapo malalamiko ya watumiaji wa huduma za mawasiliano kama simu, kuhusu changamoto wanazopata katika utoaji huduma, hata ikaamua kuchukua hatua kadhaa.

**CHANGAMOTO ZILIVYO**

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Mhandisi James Kilaba, anataja kugundua kero 10 wanazopata watumiaji mitandao ya simu, hivyo wameandaa mwongozo na kanuni ndogo zitakazosimamiwa na watoa huduma.

Ni hatua iliyoanza na kukaribisha maoni ya wadau wote kuhusu huduma ya vifurushi vinavyouzwa na watoa huduma kwa wateja.

Kilaba anasema, walilenga ufanisi unaowezesha upatikanaji huduma bora kulingana na thamani ya malipo yaliyofanywa na wanaojiunga na vifurushi husika.

Anataja la kwanza, ilikuwa kuunganishwa moja kwa moja kifurushi mara baada ya alicholipia mteja kufika ukomo wa muda au matumisi kwisha.

Pia, kuna la watumiaji kwenye vifurushi bila ridhaa yao, ikiwamo ya kutotumwa taarifa kwa mtumiaji; ikiendana na kutokuwapo uwazi wa makato ya huduma za data wakati wa kutumia vifurush na malalamiko ya watumiaji kwisha kasi ya vifurushi data.

Kilaba anasema kuna matangazo ya huduma yanayopotosha vigezo na masharti, huku upande mwingine wateja kukosa uelewa mdogo wa watumiaji kuhusu huduma na bidhaa kwenye vifurushi. Anasema, walipokea malalamiko ya watumiaji kutozwa gharama kubwa mara tu kifurushi kinapoisha, kwa kukatwa kwa salio pasipo ridhaa zao.

Lingine, ni watumiaji kupoteza muda wa maongezi, idadi ya meseji au data ambazo hawajatumia baada ya kumalizika au ukomo wa matumizi.

Mkuu huyo wa TCRAQ, anataja lingine ni shaka ya gharama kubwa kwa baadhi za huduma na kuwapo kanuni ndogo zinazohusu huduma za vifurushi na kuzitofautisha na promosheni au ofa maalum.

**MWAROBAINI WAKE**

Kilaba anasema TCRA imechukua hatua ya kuandaa mwongozo wa kanuni ndogo 12 zitakazoanza kufanya kazi rasmi tarehe Mosi, mwezi ujao ambayo wastani wa wiki tatu na nusu zijazo.

Anazitaja kanuni hizo ni toa huduma hatoruhusiwa kufanya shughuli hizo bila kibali cha TCRA; huku akipaswa kuweka utaratibu unaomuwezesha mteja aliyejiunga na kifurushi aendelee kutumia muda au uniti za kifurushi.



Mkurungezi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mhandisi James Kilaba. **PICHA: MTANDAO**

> **Dhumuni kubwa la juhudi hizi lilikuwa ni kupunguza tofauti kubwa iliyokuwapo kati ya bei za vifurushi na bei za kutumia huduma bila kujiunga na vifurushi.**

Kilaba anasema, hilo linafanyika kwa kununua salio au uniti hizo ndani ya muda wa matumizi uliowekwa, kwa kununua tena kifurushi aina hiyo hiyo kabla ya kumalizika muda wake.

Kadhalika, mtoa huduma ataweka utaratibu au mfumo unaowezesha mtumiaji huduma kuhamisha uniti za kifurushi kwenda kwa mtumiaji mwingine ndani ya mtandao wake.

Pia, mtoa huduma atapaswa kuhakikisha vifurushi zinazingatia bei husika ya chini na ya juu zilizowekwa na TCRA, pamoja na kutumia lugha, vigezo na masharti rahisi yaliyo wazi kuhusu vifurushi vinavyotolewa.

Vilevile Kilaba anasema, vifurushi vinavyotolewa kwa mtumiaji havitaondolewa, havitarekebishwa au kubadilishwa ndani ya miezi mitatu baada ya kuidhinishwa.

Nyingine anayotaja ni kwa mtoa huduma ataweka utaratibu au mfumo wa kumuwezesha mtumiaji wa huduma mwenye 'simu janja' kufuatilia matumizi ya data kwa kupakua programu ya mtoa huduma.

Mtoa huduma huyo, pia hataruhusiwa kupunguza kasi ya data kwenye kifurushi cha mteja ndani ya muda wa kifurushi husika na marufuku kufanya promosheni zaidi ya tatu au kutoa ofa maalum zaidi ya tatu kwa wakati mmoja, kupitia huduma za sauti, meseji na data.

Kwa mujibu wa Kilaba, kanuni hizo zitakapoanza kutumika, zitasaidia kujibu malalamiko mengi ya wateja yaliyopo sasa na anasisitiza, watumiaji waendelee kufuatilia mabadiliko hayo kwa umakini kwa mtazamo chanya.

"Kupitia kanuni hizi zitaboresha huduma za vifurushi kutokana na maoni ya wengi kuwa vifurushi vimekuwa vikiwasaidia," anaongeza Kilaba.

**DAWA YA MATAPELI**

Katika vita dhidi ya utapeli, Kilaba anawataka Watanzania kuendeleza mapambano ya utapeli mtandaoni, akiwataka wasome kwa kina mwongozo wa TCRA kwa watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano.

"Usikubali kutapeliwa kwa kutekeleza maelekezo yanahohusu muamala wowote wa kifedha katika simu yako, kwa kupigiwa simu na mtu yeyote anayejifanya mfanyakazi wa Kampuni yoyote ya simu au wakala wake," anasema Kilaba.

Anasema ikitokea mtumiaji wa simu amepigiwa simu au kutumiwa ujumbe mfupi wowote wa kitapeli asiutelekeze badala yake autume kwa namba 15040 pamoja na namba iliyotumia ujumbe.

**MABORESHO MENGINE**

Kilaba anasema, TCRA inachukua hatua mbalimbali ikihusisha watoa huduma, ili kushusha bei ya simu za kawaida bei nje ya vifurushi.

Kilaba anasema, kulinganisha bei hizo za kupiga simu za awali, wastani ulikuwa ndani ya mtandao mmoja pasipokujiunga na kifurushi zimeshuka kutoka Sh. 290.27 kwa dakika hadi Sh. 70.81 sawa na punguzo la asilimia 76.

Anasema wastani wa kupiga mtandao mmoja kwenda mwingine pasipo kujiunga, zimeshuka kutoka Sh. 387.55 kwa dakika hadi Sh. 71.99 kwa dakika, sawa na punguzo la asilimia 81.

Kadhalika, anasema ujumbe mfupi (SMS), zimeshuka kutoka Sh. 64.12 hadi Sh. 22.23 kwa SMS sawa na punguzo la asilimia 77.

"Dhumuni kubwa la juhudi hizi lilikuwa ni kupunguza tofauti kubwa iliyokuwapo kati ya bei za vifurushi na bei za kutumia huduma bila kujiunga na vifurushi.

Anasema, kulikuwapo malalamiko mengi kuhusu vifurushi hasa kwenye matumizi ya data, zikiwamo kutumika salio pindi kifurushi kinapofikia ukomo wa matumizi. Anasema ili kumaliza changamoto hizo Novemba 2018 mamlaka hiyo ilitoa maelekezo kwa watoa huduma kuwa simu zote za sauti kwenye vifurushi ziwe zinahesabiwa au kulipiwa kwa sekunde zilizotumika.

Anasema pia huduma za data kwenye vifurushi ziwe zinahesabiwa kwa kiwango cha kilobaiti 10 na kiwango kidogo cha kutozwa kwa data pia kiwe Kilobaiti 10.

Kilaba anawataka watoa huduma waweke utaratibu unaomuwezesha mteja anayejiunga na huduma za vifurushi, kuchagua juu ya gharama zisizokuwa kwenye vifurushi mara muda wa kifurushi alichojiunga nacho au uniti za kifurushi husika kumalizika.

"Na endapo mteja hatachagua basi asiweze kukatwa kwenye salio lake," anasema Kilaba, huku akiongeza

makadirio na kiwango cha chini cha uniti za kutozwa au kulipiwa kifahamike na kupatikana kwa mteja, ili awe na uamuzi sahihi.

"Pamoja na maelekezo hayo TCRA ilijiridhisha juu ya umuhimu wa kutengeneza utaratibu ambao kwa kiwango kikubwa utatatua kero za vifurushi, " anamalizia Kilaba.



# Jiji lalegeza masharti soko la kisasa

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imeondoa masharti magumu ya kibiashara yaliyokuwapo katika Soko Kuu la Job Ndugai ikiwamo kupunguza bei ya vizimba.

Kwa sasa bei ya vizimba hivyo ni kati ya Sh. 25,000 hadi 30,000, uamuzi huo ukifanyika kwa lengo la kuwavutia wafanyabiashara.

Hatua hiyo imetokana na kudorora kwa biashara kwenye eneo hilo huku baadhi ya vizimba vikikosa wafanyabiashara.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru, soko hilo lililoko eneo la Nzuguni, lina vizimba 365. Kati yake, 303 ndivyo vimetolewa kwa watu huku maeneo ya vibanda ghorofa ya kwanza ni 175 na yaliyotolewa ni 153.

Alisema migahawa mikubwa miwili, machinjio ya kuku na vibanda vinane vya kushushia mizigo bado havina watu.

Kutokana na hali hiyo, jiji limeondoa baadhi ya masharti yaliyokuwa magumu na kuhamisha wafanyabiashara waliokuwa Nanenane na kwenye kituo cha mabasi yanayofanya safari zake ndani ya Dodoma.

"Juhudi zote zilizofanyika zinalenga kulifanya Soko la Ndugai lichangamke na kufanya kazi kama ilivyotarajiwa," alisema.

Kiongozi huyo alisema kuwa wiki mbili zijazo, halmashauri itaanzisha gulio pembeni mwa soko na kuhamishia wafanyabiashara wa mbao ili kulifanya eneo hilo kuwa na wafanyabiashara wengi na kuongeza mvuto.

Soko hilo pamoja na kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani, ni miradi ambayo imetekelezwa kupitia Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati (TSCP) na ilikamilika Juni mwaka jana kwa gharama ya Sh. bilioni 14.6.




Mkuu wa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Decca Kampasi ya Nala, jijini Dodoma, James Ng'wandu, akipanda mti katika maadhimisho ya Siku ya Wanyamapori Duniani, chuoni hapo jana, yaliyoandaliwa na chuo hicho pamoja na Asasi ya Rafiki Wildlife, Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na Grumeti Fund, ili kuifanya Dodoma kuwa ya kijani. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Asasi yapata mbinu ya kutatua uhaba wa maji

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MWENYEKITI wa asasi za kiraia Dodoma Mjini (DUNGONET), ameishauri serikali kununua mashine za kutibu maji yenye chumvi ili yafae kwa matumizi ya binadamu hususan kwenye maeneo yenye uhaba wa maji.

Menas Muhumpa alitoa rai hiyo jana alipowasilisha taarifa za mradi wa kujenga uwezo jamii na Asasi za Kiraia (AZAKI) katika ufuatiliaji wa fedha za umma (PETS).

Mradi huo unatekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Mtandao wa Asasi za Kiraia Mkoa wa Dodoma (NGONEDO) kwa ufadhili wa The Foundation for Civil Society kwa gharama ya Sh. milioni 37.3.

Akizungumza katika kikao hicho, Muhumpa alisema katika maeneo mengi yenye upungufu, maji yamekuwa yakichimbwa, lakini hayatumiki kutokana na kuwa na kiwango kikubwa cha chumvi.

"Ni bora kukanunuliwa mashine za kutibu maji ili yafae kwa matumizi ya binadamu. Hatua hii itasaidia kutatua tatizo la maji katika maeneo mengi nchini kwani kuna visima virefu vyenye maji mengi vinachimbwa lakini maji yake hayatumiki kutokana na kuwa na chumvi nyingi.

"Niliwahi kuuliza gharama za hizo mashine, nikaambiwa zinauzwa kati ya Dola za Marekani 35,000 hadi 40, 000," alisema. Aliitaja Wilaya ya Bahi kuwa miongoni mwa wilaya ambazo maji yake yana chumvi nyingi.

Mratibu wa NGONEDO, Edward Mbogo, alisema mradi huo ulilenga kufanya mapitio na kufuatilia matokeo ya utekelezaji mradi wa PETS wilayani Bahi kwenye kata nne na kumekuwa na ufanisi mkubwa.

Alisema mradi huo unalenga kufanya mapitio na kufuatilia matokeo ya utekelezaji wa miradi ya maji, ufanisi na kero na namna ya kutekeleza miradi ya kijamii ili kuwa na matokeo chanya. Alifafanua malengo mengine mahususi ni kujua hatua zilizochukuliwa na wananchi pamoja na Halmashauri ya Bahi katika kuboresha huduma za maji kwa mtazamo wa sera na sheria ya maji.

Mbogo alitaja kata ambazo mradi huo umetekelezwa kuwa ni Bahi, Mpamantwa, Mundemu na Msisi na vijiji vinne vya Bahi, Mkakatika, Mchito na Nguji.

# RC: Kuundwe kamati kuchunguza mgogoro

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameagiza kuundwa kamati maalum ya kuchunguza mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Kijiji cha Mwegamile na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino inayodaiwa kumuuzia mwekezaji eneo lao.

Hatua hiyo ya Dk. Mahenge imefikiwa jana baada ya kufika kijijini huko na kusikiliza pande zote mbili zenye mgogoro huo.

Alisema ni vyema Katibu Tawala wa Mkoa akaunda kamati hiyo ili kubaini uhalali na eneo hilo na itafanya kazi kwa siku 14.

"Ninatoa siku 14, yaani wiki mbili kamati hiyo ije na majibu ya uchunguzini nani mwenye haki na hili eneo? Kamati ichunguze ukubwa wa eneo na uhalali wake, matumizi yaliyopo kwa sasa na baadaye na ijiridhishe madhara yanayoweza kutokea endapo eneo hilo litamegwa," aliagiza.

Alisema taarifa za awali baada ya kusikiliza pande hizo, zinadai halmashauri imetoa vielelezo ikionyesha kumiliki eneo hilo tangu mwaka 1984, lakini wawekezaji waliopewa walishindwa kuliendeleza.

Alisema kutokana na hali hiyo, wananchi walijimilikisha na kusababisha kuibuka mgogoro wakidai halmashauri inataka kuuza eneo kwa mwekezaji wakati wananchi wamekaa katika eneo hilo kwa muda mrefu.

"Hii kamati sasa ichunguze vielelezo vyote vinavyohusu eneo hili tangu wawekezaji wa awali hadi sasa. Watu wanaotakiwa kuwapo kwenye kamati ni wananchi, TAKUKURU, watu kutoka halmashauri na wajumbe kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya," alisema.

Alimwagiza mwekezaji kusitisha shughuli zote hadi hapo kamati itakapotoa majibu ya uhalali wa eneo hilo.

Awali, mwakilishi wa wananchi hao, Gabriel Masinga, alimwambia Dk. Mahenge kuwa mgogoro huo ni wa muda mrefu na waliahidiwa kulipwa fidia.

Masinga alisema kuwa hadi sasa, hakuna mwananchi aliyelipwa fidia au kufikiriwa kupewa eneo la kulima na kuchunga mifugo, hali inayosababisha kilio kikubwa kwa wananchi kwa kupoteza mashamba kwa ajili ya mradi wa kilimo cha zabibu.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa; kwenye mgogoro huu wapo wazee, watu wazima, yatima, wajane na walemavu ambao wanalia usiku na mchana kwa kadhia hii tunakupatia orodha ya wananchi walioathirika na uporaji wa ardhi ujionee mwenyewe kuwa kuna rundo kubwa la watu walioathirika na hili," alisema.

Alifafanua kuwa Januari 23 mwaka huu, walibaini halmashauri hiyo imeuza eneo lao lenye ekari 400 kwa Kampuni ya Mega Beverages Limited.

Mkuu wa Idara ya Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Godfrey Mchamale, akitoa maelezo ya halmashauri, alisema kuwa awali shamba hilo kupitia vikao halali, waliliuza kwa mwekezaji mmoja mwaka 1984 na kushindwa kuliendeleza ndipo likarudi kwenye umiliki wa halmashauri hiyo.

"Baada ya kurudi kwenye umiliki wa halmashauri, likaendelea kutumiwa na wananchi na walipotaka kuliuza kwa mwekezaji, wananchi wakadai eneo hilo ni mali yao halali.

"Mwaka 2020, halmashauri ilipitia njia zote za kuomba ekari 400 kwa ajili ya mwekezaji na wananchi walikubali kwa sharti la mwekezaji huyo kushiriki katika shughuli za kijamii na wakakubaliana ajenge shule," alisema.

Mbunge wa Chamwino, Deogratus Ndejembi, alisema wananchi hao hawapingi kujengwa kwa kiwanda hicho lakini kulikuwa na sintofahamu baada ya kuona mwekezaji ameanza baadhi ya maandalizi huku wao wakiwa hawajui lolote katika eneo hilo.





# BoT yazitaka halmashauri kuvisajili vikundi vya kijamii

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imezitaka halmashauri zote nchini kusajili vikundi vyote vya kijamii vya huduma ndogo ya fedha vilivyopo kwenye maeneo yao ili vianze kufanya kazi kwa mujibu wa sheria.

Agizo hilo limetolewa jana na Mkurugenzi wa Benki kuu Tawi la Mbeya, Ibrahim Malogoi, wakati wa mafunzo ya mfumo maalum wa kusajili vikundi vya kijamii vya huduma ndogo ya fedha yanayotolewa kwa siku tatu kwa maofisa maendeleo wa halmashauri kutoka mikoa ya Mbeya, Songwe na Rukwa yaliyofanyika jijini hapa.

Malogoi alisema kuwa Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na mamlaka imeandaa miongozo na mifumo ya usajili wa vikundi vya kijamii na huduma za kifedha.

Alisema kwa mujibu wa ratiba inapaswa vikundi vyote vya kijamii viwe vimesajiliwa ifikapo Aprili 30, mwaka huu.

"Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo maofisa maendeleo ya jamii nchini kuhamasisha vikundi mbalimbali vya kijamii kujisajili ili kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa sheria," alisema Malogoi.

Akizungumza katika mafunzo hayo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alisema kuwa baadhi ya vikundi vitoa mikopo kwa riba kubwa.

Alisema jukumu lao kwa sasa ni kufuatilia vikundi ambavyo vinatoa riba kubwa na kuwaumiza wakopaji na kwamba ni muhimu vikazingatia sheria za uendeshaji vikundi na vyama hivyo.

"Kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, tutahakikisha tunakagua vikundi vyote ili kujiridhisha kama vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria na tukibaini hawafuati maelekezo tutavifungia, lakini tutavichukulia hatua kali," alisema Ntinika.

Ofisa Maendeleo ya jamii kutoka TAMISEMI, Zahara Msangi, alisema maofisa maendeleo wa halmashauri zote nchini ndio wenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vinasajiliwa.

Benki Kuu kwa mujibu wa kifungu namba 14 wamekasimisha usimamizi huo kwa mamlaka ya serikali za mitaa na jukumu lao ni kuhakikisha vikundi vyote nchini vinasajiliwa.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Meja Jenerali mstaafu, Michael Isamuyo, akivuka mto Kiejo, ili kwenda kutembelea eneo la maji ya moto la Kiejo/Mbaka, Halmashauri ya Busokelo, mkoani Mbeya juzi, ambalo litachimbwa visima kwa ajili ya kuzalisha umeme kupitia joto ardhi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# DC aagiza kukamatwa wanaodaiwa kufanya ubadhirifu wa mil. 700/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, ameliagiza Jeshi la Polisi pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuwakamata watu 11 wanaodaiwa kufanya ubadhirifu wa Sh. milioni 700 mali ya Chama cha kuweka na kukopa cha Lulu Saccos, kilichopo Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Ntinika alitoa amri hiyo jana, wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa Chama hicho baada ya kupata taarifa ya baadhi ya watu kushindwa kurejesha fedha hizo na kuamuru wakamatwe ili walipe.

Alisema pamoja na jitihada zinazofanywa na chama hicho katika kujikwamua kiuchumi, wapo baadhi ya watu wanaokwamisha na kumuagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) kuwasaka popote pale walipo wadaiwa wa mikopo hiyo kiasi cha Sh. milioni 700. "Wadaiwa wote 11 naagiza popote pale walipo wakamatwe Sh. milioni 700 ni nyingi mno hatuwezi kuwaacha hivi hivi wazirudishe hatuwezi kuwa kama wanafunzi wa Yesu," alisema Ntinika. Akisoma taarifa ya mwaka ya chama hicho, Meneja wa Lulu Saccos, Emmy Zephania, aliomba serikali kuendelea kutoa elimu ya umuhimu wa mikopo na vyama vya ushirika.

Alisema elimu hiyo itawasaidia wananchi kukopa na kurejesha fedha kwa wakati badala ya kukopa na kushindwa kutumia fedha hizo katika malengo yaliyokusudiwa.

"Tunaomba serikali kupitia wizara zinazosimamia vyama vya ushirika vikiwamo vya akiba na mikopo, kutunga sheria za kustawisha vyama huku zikipunguza baadhi ya tozo ambazo zinawaumiza wanachama," alisema Zephania.

Baadhi ya wanachama wa Lulu Saccos walisema madeni hayo ni ya muda mrefu na wadaiwa hawataki kurejesha.

Miongoni mwa wanachama hao, Chesco Sanga, alisema uamuzi wa Mkuu wa Wilaya kuagiza wadaiwa wote kukamatwa utasaidia kujenga heshima kwa vyama vya akiba na mikopo kwa kuwa wengine watakuwa watiifu katika kurejesha fedha.

# Wanufaika TASAF washauriwa kufanya ufugaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, amezitaka kaya zote zinazowezeshwa na Mpango Taifa wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF), kujishughulisha na ufugaji wa kuku pamoja na bata wa asili kwa madai kuwa mifugo hiyo inastahimili magonjwa, lakini soko lake ni la uhakika.

Alitoa ushauri huo jana wakati wa ziara ya kuzitembelea kaya zinazonufaika na TASAF zilizopo Kijiji cha Mpakani, Kata ya Ubaruku, kusikiliza vikwazo vinavyowakabili na kuangalia shughuli wanazozifanya baada ya kunufaika na mfuko huo.

Alisema ufugaji wa bata wa asili na kuku ni miongoni mwa mifugo ambayo hutumia gharama kidogo kuendesha ikilinganishwa na mifugo mingine na kuwashauri kufuga mifugo hiyo ili kupata faida na kumudu gharama za maisha.

"Serikali itaendelea kuwawezesha wananchi kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF, kwa kuwapa mitaji elimu ya ujasiriamali na masuala mengine kwa ustawi wa uchumi wao, naamini wengi wao wamejiongeza kwa kufungua miradi ya kujiingizia pesa, nawahamasisha endeleeni kujifunza na kutafuta shughuli nyingine," alisema Mfune.

Kuhusu usimamizi na namna ya kuhudumia mifugo hiyo, alisema atawaagiza maofisa ugani kuwatembelea mara kwa mara ili kuwapa elimu ya utunzaji na kuepukana na magonjwa ikiwamo kuwahudumia vizuri na kupata soko la uhakika.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mpakani, Amos Mgongolwa alisema mara kwa mara amekuwa akiwatembelea wananchi wake kwa lengo la kuangalia shughuli za maendeleo wanazozifanya ikiwamo ujasiriamali.

Alimshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kuwatembelea wananchi wa eneo hilo na kuwapa mbinu ya ufugaji wa bata wa asili pamoja na bata ili kujiongezea kipato kupitia uwezeshwaji wa TASAF.

Miongoni mwa wanufaika wa TASAF, Bupe Mwaisumo alisema fedha za mfuko huo zimemuwezesha kufungua biashara yake ambayo kwa sasa inamsaidia kuendesha maisha yake ikiwamo kusomesha, chakula na malazi.

Alisema ana unafuu wa maisha ikilinganishwa na ilivyokuwa awali kwa kuwa licha ya majukumu ya kuendesha familia, anaweza kupata akiba na kufanya masuala mengine ya maendeleo.



## HABARI ZANZIBAR

# TAMWA yashauri wanawake waliogombea nafasi za uongozi kupata elimu ya saikolojia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA), Rose Reuben, amesema elimu ya saikolojia kwa wanawake waliogombea nafasi za uongozi hasa katika siasa inahitajika kutokana na kukumbana na vitendo vingi ambavyo huwaathiri kisaikolojia.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na umoja wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Wanawake (Juwawaza), Chukwani nje ya mji wa Zanzibar katika ukumbi wa Baraza hilo.

Alisema wanawake waliogombea nafasi za uongozi katika siasa ikiwamo ubunge, uwakilishi na udiwani, hukumbana na kashfa mbalimbali za kuwakatisha tamaa.

Alisema wapo ambao wanaathirika kisaikoljia kutokana na kashfa ambazo sio za kweli za kukatishwa tamaa ya kufikia malengo yao. "Yapo baadhi ya maneno ya kashfa huwakumba wanawake wanaogombea nafasi za uongozi hivyo ni vyema JUWAWAZA wakawapa elimu wanachama wao," alisema.

Alisema wanawake ni miongoni mwa waathirika wakuu wa unyanyasaji wa kijinsia na kuutaka umoja huo kushirikiana kupeleka ajenda ya kuvunja ukimya dhidi ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake.

Naye Mwenyekiti wa Uwawaza, Saada Mkuya, alisema ni kweli wanawake hukumbana na matatizo mengi wanapogombea nafasi za uongozi hasa katika siasa ikiwamo kashfa kwa lengo la kukatishwa tamaa.

Alisema wapo wanaodharauliwa kutokana na maumbile yao ya kijinsia na kupewa majina ya kashfa lengo likiwa ni kuwakatisha tamaa wasigombee nafasi za uongozi. "Wapo wanawake wanapogombea nafasi za uongozi hupewa maneno ya kukatisha tamaa mfano mimi mwenyewe wakati naomba kura katika mchakato wa kura za maoni wakati nilipogombea Jimbo la Kikwajuni wapo waliokuwa wameniuliza kuwa nimefukuzwa Jimbo la Welezo ambapo awali nilikuwa mbunge wa jimbo hilo laiti nisingekuwa jasiri ningeshindwa kujieleza na kuomba kura," alisema Mkuya.

Mkuya ambaye pia ni Waziri Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, alisema bado elimu inahitajika kwa jamii kuhusu nafasi za uongozi kwa wanawake ili kuwaunga mkono na kuwachagua.

Alisema umoja huo, unawajengea uwezo wanachama wake jinsi ya kusimamia sera na sheria zinazotungwa dhidi ya ukatili kijinsia katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Jimbo la Amani, Rukia Mapuri, alisema yeye ni miongoni mwa wanawake waliokumbana na maneno ya kashfa wakati alipogombea jimbo hilo.

Alisema baadhi ya jamii imekuwa na mitazamo hasi kuwa mwanamke anapoungwa mkono na mwanaume katika nafasi za uongozi kwa kuhusishwa na mahusiano na anayemuunga mkono.

"Mimi ni muhanga haswa wa hilo nilirushwa hadi katika mitandao ya kijamii kwa kashfa mbalimbali, lakini sikuvunjika moyo na nilipambana na hatimaye nikashinda katika uchaguzi mkuu," alisema.




Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Wanawake, Saada Mkuya (katikati), akizungumza katika kikao cha pamoja kati yake na uongozi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), upande wa Bara kuhusu nafasi ya mwanamke katika uongozi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ardhi yatakiwa kutafuta ufumbuzi kero za wananchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATENDAJI wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi katika kisiwa cha Pemba wametakiwa kufanya kazi kwa bidii na kuzipatia ufumbuzi kero zinazowakabili wananchi ikiwamo kutatua migogoro ya ardhi.

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Joseph Kilangi, alisema hayo wakati alipofanya ziara katika kisiwa cha Pemba kwa ajili ya kujitambulisha na kusikiliza kero za kazi.

Kilangi alisema miongoni mwa maelekezo waliyopewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi ni kuzipatia ufumbuzi changamoto za ardhi pamoja na migogoro yake.

Aliwataka watendaji hao kuhakikisha wanatenga maeneo kwa ajili ya matumizi ya ardhi ya kilimo na shughuli za makazi ya wananchi.

Alisema kumejitokeza tatizo kubwa la uvamizi wa maeneo ya kilimo kwa ujenzi wa nyumba za kudumu pamoja na kuvamiwa kwa ardhi za eka tatu tatu zilizotolewa na Rais wa kwanza wa Zanzibar hayati Abeid Amani Karume kwa ajili ya shughuli za kilimo.

"Nimekuja kwa ajili ya kujitambulisha kufuatia uteuzi wa Katibu Mkuu wa wizara hii...ombi langu kwa watendaji wa wizara kufuata sheria za kazi pamoja na kufuatilia matatizo yanayowakabili wananchi ikiwamo migogoro ya ardhi," alisema.

Naye Ofisa Mdhamini Wizara ya Ardhi, Maendeleo ya Makazi, Pemba Bakari Ali Bakari, alisema wameanza kazi ya kufuatilia eka tatu zilizotolewa na serikali kwa matumizi ya kilimo zisitumike kinyume na malengo ya awali.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili wamefanya kazi kubwa ya kuyatambua mashamba ya serikali ambayo awali yalikuwa yamefichwa kwa ajili ya matumizi kinyume na malengo.

"Tumeanza kuhakiki eka tatu za ardhi zilizotolewa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar hayati Abeid Amani Karume...lakini pia tumefanikiwa kuzifichua eka ambazo zilikuwa zikitumiwa na wananchi kinyume na sheria," alisema.

Bakari aliitaka Wizara ya Ardhi na Makazi kuzipatia ufumbuzi changamoto za bajeti pamoja na uhaba wa wafanyakazi.

Alisema wanahitaji kuajiri wafanyakazi wapya kutokana na kujitokeza kwa shughuli nyingi ambazo zinahitaji wafanyakazi zaidi ikiwamo ufuatiliaji wa mashamba ya serikali na usajili wake.

"Tunakabiliwa na changamoto ya tatizo la bajeti ndogo ambayo haikidhi malengo pamoja na uhaba wa wafanyakazi kwa ajili ya kufanya usajili wa ardhi na utambuzi wake ili kuondoa migogoro ya ardhi," alisema.

# JKU yatakiwa kuongeza nidhamu, uzalishaji chakula

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAPIGANAJI wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), wametakiwa kujenga nidhamu na kuongeza uzalishaji wa chakula ili kufikia malengo ya kujitegemea na kupunguza uagiziaji.

Mkuu wa Jeshi la Kujenga uchumi nchini, Kanali Ali Mtumweni, alisema hayo wakati akizungumza na wapiganaji kwa ajili ya kuadhimisha miaka 44 tangu kuzaliwa kwa jeshi hilo mwaka 1977.

Alisema mafanikio ya taasisi ya ulinzi ni kuimarika kwa nidhamu ambayo ndiyo utambulisho wa jeshi katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Alisema Jeshi la Kujenga Uchumi halitawavumilia wapiganaji ambao watashindwa kudhibiti nidhamu ya kazi na kulipaka matope jeshi.

"Jeshi la kujenga uchumi JKU linatimiza miaka 44 tangu kuzaliwa kwake mwaka 1977... mikakati yetu na dira iwe kulinda na kudumisha nidhamu ya kazi pamoja na kujikita katika uzalishaji wa kilimo cha mazao ya chakula," alisema.

Alisema JKU hadi sasa haijafikia malengo ya kujitosheleza kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kutumia vizuri ardhi.

"Bado hatujafanikia kujitosheleza kwa chakula licha ya kuwa na ardhi nyingi kwa ajili ya uzalishaji wa mpunga...mikakati yetu iwe kujitosheleza kwa chakula na kupunguza utegemezi," alisema.

Naye Mkuu wa JKT Divisheni ya Pemba, Meja Seif Omar Makwega, alisema wamejipanga kuimarisha uzalishaji wa kilimo kwa kutumia mabonde ya mpunga yaliopo Wete na mkoani Pemba.

Alisema licha ya kukabiliwa na uhaba wa wafanyakazi katika uzalishaji wa kilimo cha mpunga, lakini wamejipanga kuongeza uzalishaji kwa kutumia mbinu za kisasa na ushirikiano wa wataalamu kutoka Wizara ya Kilimo.

"Tumejipanga kuongeza uzalishaji wa kilimo cha mpunga kwa kutumia mashamba yetu kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Wizara ya Kilimo," alisema.

JKU lilianzishwa mwaka 1977 na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Aboud Jumbe na kupewa majukumu ya kujitosheleza kwa chakula kwa kutumia mashamba yake ya Upenja, Cheju na Mangwena huko Wete, Pemba.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ANAHITAJIKA PHARMASIA

KAMPUNI YA DAWA ILIYOPO DA ES SALAAM INAHITAJI PHARMASIA/ PHARMASIA MSAIDIZI.

KWA MAWASILIANO ZAIDI:
NAMBARI: 0713 786 300

Uza,
Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.56/2021**

Ombi la **MAIMUNA MAHAGATILA KAMBI** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **FUKANO MAGONA LUGENGE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **06/04/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo . Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 01/03/2021**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.58/2021**

**Ombi la RAPHAEL P MONGI kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu PETER REONALD MONGI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **15/03/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo . Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 03/03/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KARAGWE**
**MAOMBI NA. 139/2020**
**MURSHID ATHUMANI............MWOMBAJI**
**DHIDI YA**

1. **VICENT ROBERT KANWAKAITA**
2. **FASTO KATO PAULO**
3. **ROBERTH KANWAKAITA......WAJIBU MAOMBI**

**KWA: FASTO KATO PAULO**
**POPOTE ULIPO**

Unaarifiwa kuwa Maombi **Na. 139/2020** yamepangwa kutajwa tarehe **22/03/2021** mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, **J.K. BANTURAKI** saa 2:00 asubuhi, mahali – **KAYANGA – KARAGWE.** Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe wenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako. **AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na **MUHURI** wa **Baraza hiili leo tarehe 17/02/2021.**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
KARAGWE

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**K/SHAURINI/MSHTAKIWA/MDAIWA**
**TALAKA No. 10/2021**

**KWA: DANY MAEGA**
**WA MWANZA-TANZANIA**
**K/K. MTENDAJI WA MTAA.**

Unatakiwa kuhudhuria Mahakamani tarehe **15/03/2021** saa **3.00 asubuhi** bila kukosa kuja kujibu madai ya **NANCY WASHINGTON.** Usipo hudhuria siku hiyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yako. Hati hii imetolewa leo tarehe **04/03/2021** na muhuri wa mahakama hii.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
SONGEA

.........................................
**SAHIHI YA MPELEKEWA.**

## TANGAZO LA MNADA

**CHAMPION AUCTION MART LTD** kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD**, Tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali ya mdaiwa sugu, Ndugu Deogratias John Mwabusila ambaye ameshindwa kulipa deni lake la mkopo analodaiwa na Tujijenge Tanzania Ltd.

Mali itakayouzwa kwenye mnada wa hadhara ni kiwanja kilichopo Kitongozi cha Rukumb Vicheji - Kijiji cha Mwandege (Mkuranga)

Mnada utafanyika tarehe **19.03.2021** kuanzia saa **nne (4)** asubuhi mara baada ya gari la matangazo kupita sehemu mali husika ilipo.

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalipa 25% siku ya mnada na 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa salio halirudishwi na mnada utarudiwa.
2. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: 0756761328/0653005019 au Email:championauctionmart@gmail.com**

## KUPOTEA KWA CHETI

Kampuni ya **PETRO LOGISTICS LIMITED** iliyopo Dar es salaam inatangaza kupotelewa na cheti **(Certificate of Incentives)** chenye **namba 070667** ambacho hutolewa na Tanzania Investment Centre. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHA/RB/122963/2021** au apige **simu namba 0689 002505 / 0689 002500**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

# Kenya yaonya wasiokula mayai ya kuku kupewa chanjo corona

**Nairobi,** KENYA

TAHADHARI imetolewa kwa watu wasiokula mayai na nyama ya kuku na kupatiwa chanjo ya corona.

Kwamba chanjo hiyo, inaweza kudhuru kwa njia mbalimbali ingawaje Shirika la Afya Duniani (WHO), halijatoa mwongozo kamili kuhusu hilo.

Wizara ya Afya ya Kenya, ilitoa ilani hiyo kwa watu wasiotumia mayai na kuku dhidi ya kuipokea chanjo hiyo.

"Kuna utaratibu unaofaa kufuatwa kabla ya kupewa chanjo hiyo na iwapo unajua utapatwa na madhara ukidungwa chanjo yenye protini ya mayai au kuku, hakikisha unaiepuka chanjo hii," alisema Katibu wa Kudumu wa Wizara ya Afya, Susan Mochache.

**Serikali ya Kenya, inapanga kuwachanja takriban watu milioni moja, kutumia awamu ya kwanza.**

Hata hivyo kulingana na Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Maradhi (CDC), watu wasiotumia mayai na kuku kama chakula wanaweza kupewa chanjo hiyo chini ya mazingira ya kimatibabu, ili kushughulikia madhara yoyote yanayoweza kutokea.

Uhusiano uliopo kati ya chanjo ya corona na protini au vyakula kama mayai na nyama ya kuku ni kwamba, virusi hudungwa ndani ya protini hiyo, ili kuzalishwa zaidi na baadaye kusafishwa.

Hata hivyo hilo haliondoi kabisa kiungo cha protini kutoka chanjo yenyewe na kumdhuru yeyote ambaye hafai kula mayai au nyama ya kuku. Kulingana na mwongozo wa WHO, chanjo kwa watu walio chini ya umri wa miaka 18 haipendekezwi.

Pia kuna mjadala unaoendelea wa iwapo watu wengi watakubali kwa hiari kupewa chanjo hiyo, kwa kuwa wengi hawafahamu inavyofanya kazi, madhara ya hata kwa wasiokula vyakula hivyo.

Serikali ya Kenya, inapanga kuwachanja takriban watu milioni moja, kutumia awamu ya kwanza ya dozi zilizowasili wiki hii usiku.

Awali kulikuwa na mpango wa kuwachanja watu 500,000 kutumia shehena hiyo ya kwanza ya chanjo na dozi ya pili wiki nane baadaye. **BBC**



Mtu mmoja akiweka maua ikiwa ni kumbukumbu katika eneo hilo, watu wasiopungua watano walifariki kutokana na majeraha ya risasi siku moja kabla ya maandamano kupinga mapinduzi ya kijeshi, mjini Yangon, Myanmar, jana. **PICHA: FP**

# 28 wafariki dunia ajali gari, jengo

**Santa Cruz,** BOLIVIA

WATU 29 kati yao wanafunzi saba wamefariki dunia katika matukio mawili tofauti, ikiwamo ajali ya gari.

Katika ajali hiyo watu 21 walifariki na 20 walijeruhiwa kwenye ajali ya basi la abiria iliyotokea Bolivia.

Aidha, wengine 20 walijeruhiwa kwenye ajali hiyo.

Kulingana na taarifa za vyombo vya habari vya Bolivia, basi la abiria lililokuwa likitoka mji wa Cochabamba katikati mwa nchi, kwenda Santa Cruz, lilianguka na kutumbukia kwenye shimo la mita 150 katika mji wa Calomi baada ya dereva kupoteza mwelekeo wa usukani.

Mamlaka ilitangaza kwamba watu wasiopungua 21 walifariki dunia katika ajali hiyo na wengine 20 walijeruhiwa.

Ilibainika kuwa mmoja wa abiria aliyejeruhiwa katika ajali hiyo alikuwa Erwin Tumiri, ambaye alinusurika kwenye ajali ya ndege, iliyoanguka nchini Colombia wakati ilipokuwa ikisafirisha wachezaji wa soka wa Brazil, Novemba 29, mwaka 2016.

Tumiri, aliyenusurika katika ajali hiyo, akiwa na maumivu madogo mgongoni na magotini, alisema, "Kwa mara nyingine tena namshukuru Mungu kwa kunusurika."

Ndege iliyokuwa imebeba wachezaji soka wa Brazil ilianguka nchini Colombia, na watu watano walinusurika katika ajali hiyo, iliyojumuisha watu 81.

Pia katika tukio lingine nchini humo, wanafunzi saba walifariki baada ya kuanguka kutoka ghorofa ya nne kutokana na kukanyagana katika Chuo Kikuu nchini Bolivia.

Kwa mujibu wa habari, ajali hiyo ilitokea wakati wa mkutano wa wanafunzi katika chuo hicho.

Jukwaa lilivunjika wakati wa mkutano uliohudhuriwa na watu 60. Wanafunzi wasiopungua watano wa vyuo vikuu walianguka kutoka ghorofa ya nne na kufariki dunia. Mamlaka imeanzisha uchunguzi juu ya tukio hilo.**TRT**




Erwin Tumiri aliponusurika kwenye ajali ya ndege. **PICHA: MAKTABA**

# 38 wauawa katika maandamano

**Naypyidaw,** MYANMAR

WATU 38 wameuawa nchini Myanmar, juzi, ikiwamo wavulana wawili, walio na umri wa miaka 14 na 17, ni miongoni mwa waliouawa.

Shirika la Watoto la Save the Children, lilisema kuhusu tukio hilo na kwamba mwanamke wa miaka 19 anasemekana kuwa miongoni mwa waliouawa. Mjumbe wa Umoja wa Mataifa (UN), nchini Myanmar, Christine Schraner Burgener, alisema kuna mkanda wa video za kushtusha kutoka nchini humo.

Mashuhuda walisema vikosi vya usalama vinatumia risasi halisi na zile za mpira dhidi ya waandamanaji.

Maandamano na visa vya vurugu vimeshuhudiwa katika maeneo tofauti tangu jeshi lilipochukua madaraka Februari Mosi. Waandamanaji wamekuwa wakishinikiza kukomeshwa kwa utawala wa kijeshi na kuachiliwa huru kwa viongozi wa nchi hiyo waliochaguliwa, akiwamo Aung San Suu Kyi, aliyeng'olewa madarakani na kuzuiliwa wakati wa mapinduzi.

Uingereza imetoa wito wa kuitishwa kwa mkutano wa Baraza Kuu la Usalama la UN, huku Marekani ikisema kuwa inatafakari kuchukua hatua zaidi dhidi ya viongozi wa jeshi. **BBC**

# ICC kuchunguza uhalifu Palestina

**The Hague,** UHOLANZI

MWANASHERIA Mkuu wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC), Fatou Bensouda, ametangaza kufungua uchunguzi wa uwezekano wa uhalifu wa kivita, uliofanywa katika maeneo ya Palestina.

Februari 5, mwaka huu, ICC iliamua kwamba mamlaka yake kuongezeka hadi maeneo ya Wapalestina.

Desemba, mwaka 2019, mwanasheria mkuu wa ICC aliamua kuwa uhalifu wa kivita ulikuwa ukifanyika au ulikuwa ukifanywa katika Ukingo wa Magharibi, pamoja na Jerusalem Mashariki na Ukanda wa Gaza.

ICC ilibaini huenda wahusika wa uhalifu huo vikosi vya ulinzi vya Israeli na makundi yenye silaha ya Wapalestina kama Hamas. **RFI**

# NEYMAR ANAKARIBIA KURUDI – POCHETTINO



**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR anaendelea vizuri kupona majeraha yake, kwa mujibu wa kocha wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino.

Nyota huyo wa Brazil amekuwa nje ya dimba tangu alipoumia wakati akiichezea PSG kwenye ushindi wa Kombe la Ufaransa dhidi ya Caen, Februari 10, mwaka huu.

Maendeleo yake sasa yanaweza kumfanya awepo kwenye mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 dhidi ya timu yake ya zamani Barcelona, Machi 10, huku PSG wakiwa wanaongoza kwa mabao 4-1.

Na baada ya ushindi wa PSG wa 1-0 dhidi ya Bordeaux Jumatano, Pochettino alitoa maendeleo ya Neymar. Aliwaambia waandishi wa habari: "Kesho (leo) tutatoa picha halisi ya maendeleo yake na wachezaji wengine ambao wanaotarajia kurudi uwanjani.

"Na hili litakuwa jambo zuri kwa sababu tuna mchezo Jumamosi wa Kombe la Ufaransa dhidi ya Brest.

# Klopp aonya kuhusu usajili Liverpool

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amekubali watakabiliwa na wakati mgumu wa kuwashawishi wachezaji "bora" kusajili katika timu yake kama hawatafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Klopp alimaliza ukame wa miaka 30 wa Liverpool kusubiri kombe la Ligi Kuu England msimu uliopita, na sasa mabingwa hao watetezi wapo kwenye kiwango kisichovutia kabisa msimu huu.

Liverpool wamepitwa pointi 22 na vinara wa Ligi Kuu England, Manchester City, lakini wakiwa nafasi ya sita na wamepitwa pointi mbili kwenye mbio za kumaliza katika nne bora ili kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wekundu hao wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kuwania wachezaji kama nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland na mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, lakini Klopp ametoa onyo kuhusu usajili kabla ya mchezo wake wa jana Alhamisi dhidi ya Chelsea waliopo nafasi ya tano.

"Sababu kubwa ya kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mara zote inahusu fedha," amesema Klopp.

"Ni mashindano makubwa kucheza, lakini kwa klabu ni suala la fedha tu.

"Kwa uhakika, huwezi kuwavutia wachezaji wengine. Mwanzoni tulikuwa tunakaa na wachezaji ambao wamepewa ofa na klabu zilizofuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini sisi tutakuwa na wakati mgumu kama hatutafuzu."





# Koeman: Ni ngumu kupindua meza kwa PSG

**BARCELONA,** Hispania

RONALDO Koeman alipuuza kuzungumzia kuhusu Barcelona kupindua matokeo kwenye nusu fainali ya Kombe la Copa del Rey, wakati wakikabiliwa kuivaa Paris Saint-Germain kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Barca ilipindua matokeo ya kufungwa 2-0 kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Copa del Rey dhidi ya Sevilla kwa kuwachapa 3-0 baada ya muda wa ziada pale kwenye dimba la Camp Nou Jumatano na kutinga fainali ya mashindano hayo.

Ousmane Dembele aliwapa Barca matumaini kwa bao la kwanza la kipindi cha kwanza na golikipa Marc-Andre ter Stegen aliimarisha uhai zaidi, wakati alipookoa penalti ya Lucas Ocampos zikiwa zimesalia dakika 17 mchezo kumalizika.

Gerard Pique akafunga la pili kwa Barca na kufanya matokeo kusomeka kwa uwiano wa 2-2, wakati ambao Sevilla walipomteza Fernando aliyetolewa nje kwa kadi nyekundu.

Halafu Martin Braithwaite akaifungia bao la tatu Barca na kuwapa ushindi huo miamba hao wa LaLiga na wametangulia fainali wakimsubiri mshindi kati ya Athletic Bilbao na Levante, ambao walitarajiwa kucheza jana Alhamisi.

Barca pia wanatakiwa kupindua meza kwenye mchezo utakaopigwa Machi 10, mwaka huu kama wanataka kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwani kikosi hicho cha Koeman kilichezea kichapo nyumbani cha 4-1 kutoka kwa PSG, kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16.

Akizungumza na waandishi baada ya mchezo huo, Koeman alisema: "Kupindua meza kwa 2-0 ni rahisi, lakini kwa 4-1 ni kitu kingine kabisa.

# Arteta: Kuifundisha Barcelona ni kazi kubwa

**LONDON,** England

MIKEL Arteta hakushangazwa kuona yeye akihusishwa na kazi ya ukocha Barcelona wakati huu kuelekea kwenye uchaguzi wa urais pale Camp Nou, utakaofanyika Jumapili hii.

Kocha huyo wa Arsenal anafikiri kwamba, kutokana na mahusiano yake ya karibuni na Barca, ambako alianzia kucheza soka, alitarajia hilo.

Hata hivyo, Arteta alisisitiza kwamba kwa sasa akili yake "leo na kesho" ni kuendelea kuinoa Arsenal.


Arteta alishinda taji la FA na Ngao ya Jamii mapema ndani ya miezi yake ya kwanza klabuni hapo, licha ya kwamba, sasa ana wakati mgumu kwenye Ligi Kuu England.

Arsenal wapo nafasi ya 10 katika msimamo wa Ligi Kuu England na Jumapili hii itakuwa ugenini kucheza dhidi ya Burnley, wakitoka kupata ushindi mzuri dhidi ya Leicester City.

Washikabunduki hao pia tayari wamefuzu Ligi ya Europa hatua ya 16 na Arteta amebainisha kwamba kuna kazi nyingi za kufanya.

"Mara zote lazima kuwe na uvumi wakati Barcelona wakiwa kwenye uchaguzi," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari, baada ya madai kwamba, mgombea urais, Joan Laporta anataka kumchukua akishinda nafasi hiyo.

"Ni timu kubwa. Bila shaka yoyote nililelewa pale na kukua kama mchezaji na mara zote wamekuwa na uhusiano mzuri."





# DE GEA, MARTIAL HATIHATI KUIKABILI MAN CITY

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United ina uwezekano wa kuwakosa golikipa wake, David de Gea na Anthony Martial kwenye mchezo wa 'dabi' ya Jumapili dhidi ya vinara wa Ligi Kuu England, Manchester City.

Si De Gea wala Martial waliosafiri kwenda jijini London na timu hiyo kwa ajili ya mchezo wa juzi Jumatano dhidi ya Crystal Palace, pale katika dimba la Selhurst Park.

Dean Henderson alianza, huku Lee Grant akiwa chaguo la pili kwenye mchezo huo kutokana na kukosekana kwa De Gea kwa sababu binafsi. Kocha Ole Gunnar Solskjaer aliwachagua Marcus Rashford, Mason Greenwood na Edinson Cavani, kwa sababu Martial alikuwa majeruhi baada ya kuumia kwenye mazoezi.

Haijajulikana kama wawili hao watakuwapo kwenye mchezo huo dhidi ya City utakaopigwa pale kwenye dimba la Etihad.

"David, ana sababu binafsi," alisema Solskjaer akiiambia MUTV kuhusu kukosekana kwao.

"Anthony aliumia goti Jumatatu kwenye mazoezi, hivyo hakuwa tayari kwa mchezo wa Jumatano. Matumaini yetu anaweza kuwapo kwenye mchezo wa Jumapili, lakini hatuna uhakika bado."

# *Madrid yashikilia hatima ya Bale*

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho amesema ni juu ya Real Madrid kama watamruhusu fowadi wa Wales, Gareth Bale kubakia hapo Spurs msimu ujao.


Bale mwenye umri wa miaka 31, anacheza hapo kwa mkopo akitokea Real na amebakiwa na msimu mmoja kumaliza mkataba wake na miamba hao wa Ligi Kuu ya Hispania.

"Sio mchezaji wa Tottenham, hivyo Real Madrid wana kila kitu mikononi mwao," amesema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari.

"Mimi nina mchezaji ambaye yupo kwa mkopo na najaribu kumfanya kuwa kama mchezaji wa Tottenham Hotspur."

Aliongeza: "Tunajaribu kumhudumia vizuri mchezaji ambaye yupo kwa mkopo, lakini kwa heshima ya klabu ambayo inamtoa mkopo mchezaji.

"Kama ukitaka kuuliza chochote kuhusu majaliwa ya Gareth unatakiwa kumuuliza kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER AJIPANGA KUMZUIA FERNANDES

**Kusafiri kwenda Ureno kuitumikia nchi yake kutokana na sheria mpya zilizowekwa na...**

**LONDON,** England

OLE Gunnar Solskjaer anafikiria kama amzuie nyota wa Manchester United, Bruno Fernandes kusafiri na Ureno kwa ajili ya mechi za kimataifa, kutokana na karantini ya corona.

**Ureno imepangwa kucheza mechi mbili za kufuzu Kombe la Dunia mwezi huu – nyumbani dhidi ya Azerbaijan (Machi 24), ugenini dhidi ya Serbia (Machi 27) na Luxembourg (Machi 30).**

Kama akijiunga na kikosi cha Ureno maana yake ni kwamba, Fernandes akirudi England atatakiwa kukaa karantini kwa siku 10 kwa mujibu wa sheria zilizowekwa na serikali ya Uingereza kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Hiyo itamwacha Solskjaer bila huduma ya Fernandes kwenye mchezo dhidi ya Brighton and Hove Albion (Aprili 3) na Tottenham (Aprili 10).

Alipoulizwa kuhusu hilo baada ya sare ya bila kufungana ya Jumatano ya ugenini dhidi ya Crystal Palace, kocha huyo wa United, Solskjaer aliwaambia waandishi wa habari: "Hatujakaa chini na kuamua nini cha kufanya.

"Kumpoteza mchezaji kwa siku 10 akiwa amejitenga ni jambo gumu kwetu, na sisi ndio tunaowalipa wachezaji, kwa kile ninachokielewa, lakini haina maana kama unampoteza mchezaji kwa siku 10.

"Namtaka Bruno kuwa tayari kwa mchezo dhidi ya Brighton na matumaini yangu tutafuzu Ulaya na dhidi ya Tottenham baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa, bila shaka yoyote."

United walipata sare yao ya tatu mfululizo kwenye mashindano yote, baada ya kukamatwa na Palace, Jumatano pale katika dimba la Selhurst Park, ambapo sasa wamepitwa pointi 14 na vinara Manchester City, kuelekea kwenye mchezo wao wa 'dabi' ya jiji moja Jumapili.

## ZISIKUPITE

### SITA ZAMTAKA HAALAND

NYOTA anayewaniwa na Chelsea, Erling Braut Haaland, 20, wa Borussia Dortmund amesema kuna klabu sita ambazo anaweza kufikiria kujiunga nazo, huku Liverpool, Manchester United na Manchester City zikiwa timu pekee kutoka Ligi Kuu England. ***(Bild, via Sun)***

### KEHL: HAALAND HAONDOKI

KLABU ya Borussia Dortmund inapanga kumbakiza nyota wake, Erling, Haaland (20), baada ya msimu wa kipindi cha majira ya joto, kwa mujibu wa kocha mkuu wa kikosi cha kwanza, Sebastian Kehl. ***(London Evening Standard)***

### ARSENAL YASAKA WAWILI

ARSENAL inafikiria kuwasajili, mlinzi wa Brighton, Tariq Lamptey mwenye umri wa miaka 20, na beki wa pembeni wa Norwich, Max Aarons (21), kuziba nafasi ya mlinzi wa kulia, Hector Bellerin mwenye miaka 25, ambaye anahusishwa sana na Paris St-Germain. ***(Sun)***

### CHELSEA KUNUFAIKA

CHELSEA watapata asilimia ambayo haijatajwa kama ada yoyote italipwa kumnunua beki wa Brighton, Tarig Lamptey mwenye miaka 20, kutokana na kipengele cha mkataba kilichowekwa wakati nyota huyo akitoka pale Stamford Bridge Januari, mwaka jana. ***(Express)***

### AGUERO ATAKIWA BARCA

MGOMBEA urais wa Barcelona, Joan Laporta amebainisha kwamba, fowadi wa Manchester City na Argentina, Sergio Aguero mwenye miaka 32, atamsajili kipindi cha majira ya joto, kama akishinda uchaguzi. ***(Mail)***

### ARTETA AIKATAA BARCA

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema akili yake ni kuendelea kuifundisha Arsenal, licha ya kuhusishwa kutakiwa na vigogo wa Hispania, Barcelona. ***(ESPN)***

### LACAZETTE MAMBO SAFI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema mazungumzo na straika Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2023, yataanza hivi karibuni. ***(Mail)***

### YOUNG KUREJEA WATFORD

WINGA wa zamani wa England, Ashley Young mwenye umri wa miaka 35, ana matumaini kubeba taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, akiwa na Inter Milan kabla ya kurudi katika klabu yake ya kwanza ya Watford akiwa mchezaji huru. ***(Mirror)***

### KLOPP AFUNGUKA

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amedai Liverpool itakuwa na wakati mgumu kusajili wachezaji nyota, kama hawatafuzu kucheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Goal)***

# Corona yakimbiza netiboli Mashariki

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Netiboli ya Afrika Mashariki yaliyotarajiwa kufanyika Aprili, mwaka huu, nchini Uganda hayatafanyika tena kutokana na ugonjwa wa corona ambao bado unaendelea kuyatesa mataifa mbalimbali duniani.

Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Devotha Marwa (pichani chini), aliliambia gazeti hili mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka hayatakuwapo na hivyo wachezaji wanatakiwa kuendelea na programu nyingine.

"Hatuwezi kuingia gharama za kuweka wachezaji kambini kwa kuwa hali sio nzuri, hivyo tutaendelea kucheza mechi za kirafiki baada ya kumalizika kwa mashindano ya Ligi za Mikoa na Wilaya," alisema Marwa.

Mwenyekiti huyo alisema ugonjwa huo umewavurugia ratiba yao kwa sababu wenyeji Uganda hawajatuma taarifa yoyote kuhusiana na michuano hiyo.

"Bado tunakabiliwa na changamoto ya ugonjwa huo mkubwa, tunawaomba wachezaji wetu pamoja na Watanzania kujihadhari na ugonjwa huo kwa kufuata taratibu za wataalamu wa afya ili tusipoteze nguvu kazi," Marwa alisema.

Alisema walitarajia mashindano ya mwaka huu kuwa na ushindani zaidi kwa sababu idadi ya nchi shiriki ziliongezeka baada ya Burundi, Sudan, Zimbabwe na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kuomba kushiriki.



# BOCCO AISHUKURU SBL KUIUNGA MKONO STARS

**Na Mwandishi Wetu**

NAHODHA wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), John Bocco, ameishukuru Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kwa kuendelea kuiunga mkono timu hiyo hata baada ya kuondolewa mapema katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

**SBL ndio mdhamini mkuu wa Taifa Stars kupitia bia yake aina ya Serengeti Premium Lager.**

Akizungumza na gazeti hili, Bocco alisema SBL imekuwa bega kwa bega na Stars na kuongeza pamoja na kuwa timu hiyo haikuweza kufanya vizuri CHAN, bado kina ari kubwa na pia kinamatumaini ya kufanya vizuri katika michuano iliyopo mbele yake ikiwamo kufuzu AFCON 2022 pamoja na Kombe la Dunia litakalofanyika nchini Qatar 2022.

"Tunawashukuru wadhamini kwa kuwa kupitia udhamini wao tuliweza kufuzu kucheza fainali za CHAN. Pamoja tumetolewa katika hatua za mwanzoni, SBL bado wameendelea kuwa na timu na huku wakitupa moyo na hii inasaidia kujenga ari na morari ya kikosi," alisema Bocco.

Nahodha huyo alisema Stars ina mambo mengi ya kujivunia chini ya udhamini wa Serengeti na kutaja moja kati ya hatua kubwa ambayo timu hiyo iliifikia ni kufuzu kushiriki mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2019), ikiwa ni baada ya miaka 39.



"Pasipo udhamini mzuri wa SBL ambao uliiwezesha timu kujiandaa ipasavyo na kufanya vyema katika mechi zake pengine isingekuwa rahisi kufuzu kucheza mashindano haya makubwa kuliko yote barani Afrika," alisema Bocco.

Katika michuano ya CHAN iliyomalizika, Stars ilikuwa katika Kundi D pamoja na timu za Zambia, Guinea na Namibia na ili kuendelea kusonga mbele ilihitaji kuifunga Guinea ikiwa ni baada ya kufungwa na Zambia na kuifunga Namibia.

Hata hivyo, matarajio ya timu hayakwenda vizuri baada ya kulazimishwa sare ya 2-2 na timu ya taifa ya Guinea. Katika mechi yake na Guinea, Taifa Stars ilifanikiwa kuongoza kwa mabao 2-1 hadi kufikia dakika ya 70 ya kipindi cha pili kabla ya Guinea kusawazisha na kuzima ndoto za Stars kusonga mbele.

Mkuu wa Kitengo cha Bia wa SBL, Anitha Msangi, alisema pamoja na kushindwa kusonga mbele, kikosi kilijitahidi na kuonyesha kiwango kizuri kikishuhudiwa na ushindi dhidi ya Namibia na kandanda safi dhidi ya Guinea.

"Bia ya Serengeti ikiwa kama mdhamini mkuu wa Stars bado tunajivunia mafanikio yake yaliyopita na ya sasa. Tunaamini timu ina nafasi nzuri ya kufanya vyema katika michuano ijayo, sisi kama wadhamini tupo nyuma yao kuwapa nguvu," alisema Msangi.

Alisisitiza bia ya Serengeti itaendelea kuisaidia Stars kusonga mbele kulingana na mkataba wa miaka mitatu iliyoingia na Shirikisho la Soka Nchini (TFF).

Mwaka jana SBL ilisaini mkataba mpya na TFF ambapo ilikubali kuongeza udhamini kwa miaka mitatu mingine badaa ya mkataba wa awali uliosainiwa mwaka 2017 kumalizika muda wake.

Katika hafla ya utiliaji sahihi, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alinukuliwa na vyombo vya habari akisema SBL kupitia bia ya Serengeti iliamua kusaini mkataba mpya baada ya kuridhishwa na mwenendo wa timu hiyo.




Mshindi wa bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Juma Chingomanje (34), kutoka Sirari mkoani Mara akiwa ameshika mfano wa hundi ya Sh. milioni 11.4 ambayo ni zawadi aliyopata baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita kwa dau la Sh. 2000 tu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga Princess, Simba Queens majaribuni*

**Na Saada Akida**

WATANI wa jadi nchini, Yanga Princess inatarajia kuwakaribisha Simba Queens katika mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Yanga inashuka dimbani ikiwa ndio vinara wakati Simba Queens wao ni mabingwa watetezi na wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo huku wakiwa na kumbukumbu ya kutoka suluhu katika mechi ya mzunguko wa kwanza.

Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, alisema wamejiandaa vizuri na wachezaji wake wako fiti kwa ajili ya mchezo huo ambao wanahitaji pointi tatu muhimu.

"Tunawaheshimu Simba Queens, tumejipanga kwenda kutafuta matokeo mazuri kwa ajili ya kujiimarisha katika nafasi ya kwanza katika msimamo wa ligi, mechi hiyo inaweza kutoa taswira ya ubingwa wa msimu huu," alisema Edna.

Naye Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema wamefanya maandalizi kwa asilimia 90, sasa wanasubiri kumaliza kazi uwanjani.

Nahodha wa Simba, Mwanahamisi Omar 'Gaucho' alisema makocha wamemaliza kazi yao na sasa jukumu limebakia kwao kutafuta matokeo mazuri.

"Hatutaogopa ubora wa Yanga, tumejipanga kwenda kutafuta matokeo mazuri katika mchezo wa kesho (leo), kwani tunahitaji pointi muhimu ili kumshusha mpinzani, kwa sababu wao wako nafasi ya kwanza na sisi tuko nafasi ya pili, tukiwa nyuma ya pointi mbili," alisema Gaucho.

# Michezo

Ijumaa Machi 5, 2021

Nipashe




Solskjaer ajipanga kumzuia Fernandes

UKURASA 22



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Abdulrazack (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa Coastal Union, Paschal Kitenge katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga jana. Coastal ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

## Simba SC yatamba Merrikh hawatoki

**Na Mwandishi Wetu,** SUDAN

TUNASUBIRI muda! Hayo ni maneno ya wawakilishi wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba kuelekea mchezo wa hatua ya makundi dhidi ya wenyeji Al Merrikh utakaochezwa kesho jijini Khartoum nchini Sudan.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri na wanachosubiri ni muda wa kukamilisha jukumu lililowapeleka Sudan kufanyika. Manara alisema wanawashukuru wenyeji wao kwa mapokezi mazuri na hiyo ni dalili nzuri kwamba watahakikisha wanapambana na kupata matokeo chanya katika mechi hiyo ya tatu ya Kundi A.

"Kila kitu kiko sawa, wachezaji waliamka salama, ninachowaambia Wanasimba na Watanzania kwa ujumla, cha msingi niwaarifu, Wasudan wametupokea vizuri, tumepokewa kwa heshima, kila kitu kinaenda vizuri, tunawasubiri Merrikh siku ya Jumamosi hawatoki," alisema Manara.

Aliongeza wachezaji wao wote walifanyiwa vipimo vya COVID-19, na anaamini majibu yatatoka vizuri kwa ajili ya kukamilisha maandalizi ya mwisho wa mchezo huo.

Kocha Msaidizi wa Simba, Seleman Matola, aliliambia gazeti hili wamejiandaa kukutana na mechi ngumu na yenye ushindani kwa sababu wapinzani wao wamepoteza mechi mbili za kwanza walizocheza.

Matola alisema msimu huu wamejipanga kufanya vizuri katika mashindano hayo ya kimataifa na wamewaeleza wachezaji wao watumie mechi hizo kujitangaza.

"Pia Gomes (Didier- kocha wa zamani wa Al Merrikh), kuwa ndani ya Simba ni miongoni mwa sababu ambazo zitaongeza ugumu kwenye mchezo huo, wao hawana presha tofauti na sisi ambao tuna pointi na tunahitaji kushinda, watakuwa na presha kubwa ya kutaka kushinda ili kulipa kisasi kwa mwalimu wao kuondoka," alisema Matola.

# Rekodi ya Yanga yavunjwa Tanga

## Kaze ana kazi baada ya kuchapwa mabao 2-1 na Coastal Union katika mechi...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kucheza mechi 21 bila kupoteza, hatimaye vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, jana Yanga wamepoteza mchezo wao wa kwanza msimu huu, ikifa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga kwa mabao 2-1 dhidi ya wenyeji wao Coastal Union.

**Alikuwa ni Mudathir Abdallah aliyepeleka majonzi Jangwani na kutibua rekodi nzuri ya Yanga msimu huu dakika ya 83, alipofunga bao kwa shuti kali akiwa pembeni, nje kidogo ya eneo la hatari, lililomshinda kipa, Farouk Shikalo na mpira kujaa wavuni.**

Zilikuwa ni juhudi zake mfungaji huyo baada ya kuwalamba chenga mabeki wa Yanga, kabla ya kufumua shuti hilo.

Mkosi kwa Yanga ulianza mapema dakika ya nane ilipokosa mkwaju wa penalti kupitia kwa Tuisila Kisinda iliyotokana na Fiston Abdulrazack kukwatuliwa na beki Salum Ally, lakini uliishia mikononi kwa kipa wa Cosatal Union, Aboubakar Abbas.

Dakika mbili tu baadaye, Coastal Union iliandika bao kupitia kwa Erick Msagati aliyepiga shuti akiwa ndani ya eneo la hatari, goli likiwa tupu, baada ya Shikalo kuufuata mpira wa faulo pembeni uliopigwa na Hassan Kibailo, lakini ulimgonga mchezaji mmoja wa Coastal na kumkuta mfungaji.

Feisal Salum 'Fei Toto' nusura aisawazishie Yanga bao dakika ya 19, baada ya shuti lake la kushtukiza kumbabatiza kipa Abbas na kuzagaa kwenye eneo la hatari, kabla ya kipa huyo kuuwahi na kuudaka tena.

Yanga ilifanya mabadiliko dakika ya 32 ya mchezo, Michel Sarpong akitoka na nafasi yake kuchukuliwa na Yacoub Songne, ikiwa ni mechi yake ya kwanza baada ya muda mrefu kuwa majeruhi.

Iliwachukua dakika mbili tu Yanga baada ya Songne kuingia, Tuisila akisawazisha makosa yake ya kukosa penalti, aliposawazisha bao, kutokana na makosa ya mabeki wa Coastal Union kutojipanga vyema, mfungaji akiwazidi ujanja na mbio, kabla ya kushuti lake kwa kwanza kumbabatiza Abbas na ukamrudia tena mfungaji, akaujaza wavuni.

Farid Mussa alikosa bao la wazi, akiwa yeye na kipa, alipowazidi mbio mabeki wa Coastal Union, kwa mshangao wa wengi wakidhani mpira huo unakwama wavuni, lakini ulitoka nje kidogo la lango.

Kipindi cha pili licha ya timu zote kufanya mabadiliko, lakini soka lililochezwa lilikuwa ni lile lile la pasi ndefu na kukimbizana, huku kukiwa na matumizi makubwa ya nguvu.

Deus Kaseke aliikosesha Yanga bao dakika ya 71 ambaye aliingia kuchukua nafasi ya Farid, alipopiga shuti kali likatemwa na kipa, na mabeki wa Coastal Union waliufagia kabla ya wachezaji wa Yanga kuufikia.

Kuanzia dakika ya 70 hadi 80, Yanga ilihamia kwenye lango la Coastal Union kwa kufanya mashambulizi, lakini mabeki wa Coastal, Kibailo, Hance Masoud, Peter Mwangosi na Mkongomani, Paschal Kitenge walikaa imara kuokoa mashambulizi hayo, kabla ya bao la pili kupatikana dakika nane kabla pambano hilo kumalizika.

Kwa matokeo hayo, Yanga imebakia na pointi zile zile 49, lakini ikiwa imecheza mechi 22, huku wanaoshika nafasi ya pili Simba ikiwa na pointi 45 kwa mechi 19 wakati Coastal Union yenyewe imepaa kutoka nafasi ya 15 hadi ya 10 baada ya kufikisha pointi 26, ikicheza mechi 22.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >